Ijumaa Mei 22, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580238
www.ippmedia.com
The Guardian digital   nipasheTZ   nipasheTZ   nipasheTZ   0745 700710



## Wabunge wapewa notisi kutoka nyumba za serikali

UKURASA 3



Simulizi ndoa kuvunjika na kulipuka umasikini kifamilia

BUFE

IJUMAA MEI 22, 2020 Nipashe BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Ijue Saccos iliyokamata walimu na watumishi umma Missenyi, Bukoba

BIASHARA

Mwenyekiti Mkuranga ang'aka 'amcos' kuamua bei peke yake

• DC: Tunadaiwa Sh. bn. 1 za korosho; Sh. 33 dalili 'kupigwa'

Na Yasmine Protace, Mkuranga

Sehemu ya korosho ikiwa ghalani Mkuranga, ikifanyiwa ukaguzi na uongozi wa serikali mwaka jana. PICHA: MTANDAO.

"Katika mwaka wa fedha 2017/2018, walikusanya jumla ya Sh. bilioni 6.3; mwaka 2019/2020 walifikisha Sh. bilioni 6.5.

DC AFAFANUA

DED NA MAPATO

UKURASA 11

# Magufuli afungua vyuo, kidato 6

**AAGIZA** uchunguzi vifaa kinga corona, vitakavyokuwa na tatizo kushtakiwa jinai ya mauaji...*Endelea ukurasa 2*




Rais John Magufuli, akizungumza na viongozi aliowaapisha katika Ikulu ya Chamwino, mkoani Dodoma jana.
**PICHA: IKULU**

## BAA LA CORONA



Ushauri wa Shirika la Afya Duniani (WHO), mazoezi kwa watu wenye umri mkubwa yanasaidia kuboresha uimara wa misuli kujilinda wasianguke ovyo na kupata majeraha. Kwa watoto, mazoezi ya kila siku yanasaidia kuimarisha afya na ukuaji, kupunguza hatari ya kupata magonjwa na pia kuwajengea uwezo wa uhusiano kijamii. Kipindi hiki cha corona ni muhimu kufanya mazoezi.

* **Epuka mikusanyiko ya watu**
* **Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka**
* **Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana**
* **Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo**

## Watalii waanza kuingia nchini



UKURASA 3

## DIWANI KORTINI SHTAKA RUSHWA MILIONI 1/-

UKURASA 3




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play   Download on the App Store


MICHEZO LIGI KUU BARA YAREJEA RASMI UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

**HABARI KITAIFA**

# JPM afungua vyuo, kidato cha sita

**Na Romana Mallya**

RAIS John Magufuli ametangaza kuanzia Juni Mosi, vyuo vyote pamoja na kidato cha sita vitafunguliwa na kuwaagiza watendaji wake ndani ya siku tisa kuandaa mikopo kwa ajili ya wanafunzi wa vyuo.

Machi 17 mwaka huu, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alitangaza kufunga shule zote za awali, msingi na sekondari na baadaye vyuo vyote kwa muda wa siku 30 kutokana na janga la corona.

Akizungumza jana Ikulu ya Chamwino mkoani Dodoma wakati akiwaapisha viongozi mbalimbali aliowateua hivi karibuni, Rais Magufuli alisema ameamua kufungua vyuo kwa sababu maambukizo ya corona yamepungua.

"Kutokana na hali kwenda vizuri, tumeamua vyuo vyote vifunguliwe Juni Mosi, niwaombe wizara zinazohusika, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Wizara ya Fedha na Mipango ambayo inahusika kwenye kutoa mikopo kwa ajili ya wanafunzi. Leo (jana) ni Mei 21, tuna siku tisa.

"Wizara hizi zinazohusika, Wizara ya Elimu na Wizara ya Fedha zijiandae ili vyuo vitakapofunguliwa, kusiwe na kero nyingine, kama mwanafunzi anastahili kupata, mkopo wake uwe umeandaliwa mapema," aliagiza.

Rais alisema siku tisa kwa wizara ambayo ipo makini, haiwezi kushindwa kumaliza na kufanya maandalizi na ndiyo maana ameamua kutangaza mapema ili ndani ya siku hizo wajipange.

Aliagiza wanafunzi wa kidato cha sita ambao wanajiandaa kwa ajili ya mitihani yao ya mwisho, nao watarudi kwenye shule zao kuanzia Juni Mosi.

"Wizara ya Elimu ipange vipindi ili wafanye mtihani wao bila kuharibu mwenendo wao wa kuingia vyuo vikuu kama ilivyopangwa, corona usiwachelewweshe," aliagiza.

Kuhusu shule za msingi na sekondari, Rais Magufuli alisema wameona watoe muda zaidi kwa sababu wanafunzi walioko katika ngazi hiyo ya elimu ni wadogo, hivyo kuna haja nchi kujipa nafasi kadri wanavyopambana na corona.

**NDEGE ZA WATALII**

Rais Magufuli pia alisema serikali imeamua kuanzia Mei 27 na 28 mwezi huu, ndege za watalii zitaanza kuingia nchini na hawatawekwa karantini kwa siku 14.

"Bahati nzuri wapo wengi ambao wameomba kuja, kuna mashirika mengine yamejaa karibu mwezi Agosti, hatuwezi kuiachia fursa hii na kuendelea kujifungia wakati wao wanaona sehemu za kustarehe ni huku.

"Na utalii mwingine wanaweza kufanya huo wa nyungu kama alivyoeleza (Seleman) Jafo (Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa - Tamisemi) nao ni utalii wa aina yake.

"Utalii siyo kuona wanyama tu, hata mtu kujifukiza na akanywa dawa za kienyeji na kupona, inawezekana ikawa sekta moja wapo ya kusaidia watu waliokaa kule wamefungwa kwa miezi, wanakuja Tanzania kuona jua na utukufu wa Mungu na wanyama walivyo," alisema.

**HALI YA CORONA**

Rais Magufuli alisema hali ya maambukizo imeshuka, akitolea mfano Mkoa wa Singida ambao una wagonjwa watatu tu wanaosubiri vipimo vya mwisho, ili watoke hospitalini.

"Nimetembea kwa gari kutoka Mkoa wa Geita mpaka Dodoma, njiani watu wanajishughulisha na shughuli zao, wanalima, hiki ndicho tunataka kwa ajili ya kujenga uchumi wetu," alisema.



Abiria wakionekana kuanza kustaarabika na kupanga foleni wakati wa kuingia kwenye daladala, Kituo cha Mbezi Mwisho, jijini Dar es Salaam jana, tofauti na awali ambapo walikuwa wakigombea na kusukumana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# ...aagiza vifaa kinga vichunguzwe

**Na Romana Mallya**

RAIS John Magufuli ameagiza vifaa vinavyotolewa kama msaada kwa ajili ya kujikinga na virusi vya corona vipokewe na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na kuchunguzwa kama havina virusi kabla havijatumika.

Aliyasema hayo jana Ikulu Chamwino mkoani Dodoma, alipowaapisha viongozi mbalimbali aliowateua hivi karibuni na kuagiza endapo vifaa hivyo vikikutwa na maambukizo ya corona, wahusika washitakiwe kwa jinai ya mauaji.

Rais Magufuli alilifafanua kuwa juzi aliona Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) ikipokea vifaa vya kujikinga na corona.

"Kama ni kupokea kifaa chochote cha kupambana na corona, lazima kipitie Wizara ya Afya na kifanyiwe uchunguzi, siyo mtu amekaa huko ana kitaasisi chake, tunaomba michango mingine ya watu ya kupambana na corona, kuna mahali fulani walikuwa wanaitisha mradi tukachangeni, hapana.

"Ninaawaomba Wizara ya Afya, Naibu Waziri (Dk. Godwin Mollel) upo hapa, Waziri Ummy, Katibu Mkuu, mkasimamie hili. Mtu yeyote atakayepewa vifaa vya corona, halafu mkapima na kukuta vina corona, huyo mtu apelekwe kwenye kesi ya jinai hata ya mauaji kama wauaji wengine," aliagiza.

Aliwatahadharisha watendaji serikalini kuhusu kile alichokiita 'kupokea pokea', akikumbusha kuwa tayari Waziri Ummy ameshaomba fedha ili barakoa zitengenezwe nchini.

"Tutanunua vifaa ambavyo tunajua vimepimwa kwenye maabara zetu na kujua hiki ni kifaa kweli ninachofaa kwa ajili ya matumizi ya Watanzania," alisema.

Rais Magufuli alisema ugonjwa wa corona ni vita na katika misaada, huenda wananchi wakapewa barakoa zenye corona.

"Mwenendo wa maambukizo unakwenda vizuri kutokana na hatua tunazozichukua, yapo mengi tunayoyachukua, mengine hatuyatangazi. Vya bure vibaya, ndiyo maana tunaipongeza Wizara ya Afya kwa kazi nzuri iliyofanya chini ya Waziri wake, Ummy Mwalimu," alisema.

Rais Magufuli aliipongeza wizara hiyo na watendaji wengine kwa kuwa sasa barakoa zinashonwa Tanzania na Jeshi la Wananchi linafanya kazi nzuri, huku Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH) ikishona vazi maalum kwa watoa huduma za afya kujikinga (PPE) kwa gharama nafuu.

"Nilifikiri fedha za mfuko wa Global Fund zitumike kutengeneza vifaa vyetu wenyewe, kwanza zitajenga ajira na kuokoa na zitatumika kwa watu wengi," alisema.

Rais aliwataka Watanzania wachukue tahadhari kubwa kwa sababu maambukizo ya corona nchini yanashuka chini na yanaelekea kuisha.

"Lakini, tusije tukapandikiziwa corona kwa uzembe wetu au kwa uzembe wa mtu yeyote, mtu akitaka kusambaza msaada hatukatai, peleka Wizara ya Afya, pale kuna wataalamu watakichunguza kifaa, mkalisimamie hili, dezo zinaua.

"Tunahitaji misaada na tunawashukuru sana kwa ambao wameamua kutusaidia kwa mfano wanaotusaidia kwenye elimu kama ulivyozungumza Profesa (Waziri wa ELimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Joyce Ndalichako), wafikishie salamu nchi ya Canada, European Union (Nchi za Umoja wa Ulaya) na wengine ambao wanajitolea kutusaidia," alisifu.

**AMSIFIA WAZIRI UMMY**

Rais Magufuli pia alisema Waziri Ummy anastahili pongezi kutokana na kujituma katika janga hilo la corona, akibainisha kuwa 'amesimama kweli' licha ya kwamba hana taaluma ya udaktari.

"Kuna wakati fulani niliona anasimama peke yake kwenye wizara, yeye siyo daktari wa kusomea, unajiuliza mwanasiasa anasimama peke yake kuzungumzia taaluma ya udaktari, wasaidizi wake wote ni madaktari huoni matokeo, ninakupongeza sana Ummy, ninajua nilikutesa.

"Sitaki kueleza mengi, lakini ni kweli aliteseka kwa sababu kwa siku mara nyingine alikuwa anapigiwa simu zaidi ya mara nane, iwe saa nane iwe saa ngapi, unapokuwa kwenye vita, saa nyingine kubembelezana hapana," alisisitiza.

Rais Magufuli alisema Waziri Ummy alisimamia wizara hiyo kwa ujasiri mkubwa na kumtaka Naibu Waziri mpya, Dk. Mollel aende kumsaidia.

"Kwa mfano Mollel kwenye jimbo lako hospitali ikajengwa na kumalizika halafu usipeleke dawa, hapo kwenye jimbo lako usipeleke madaktari, wewe upo.

"'Message sent' (ujumbe umefika), mshikamano unaanzia nyumbani, unapopewa jukumu lazima utimize wajibu," alisema.

**MAGEREZA YABADILIKA**

Rais Magufuli pia alisema baada ya kufanya mabadiliko Magereza, Kamishna Jenerali wa Magereza, anafanya kazi na katika kipindi cha miezi mitatu, hajaomba fedha serikalini kwa ajili ya kulisha wafungwa.

"Wale waliokuwapo wa vyeo vyeo waliokuwa wanamsumbua kidogo, akaandika barua huku napo ikacheleweshwa, baadaye nikamwambia Katibu Mkuu Kiongozi shughulikia, ninafikiri umelishughulikia wale mmeshawahamisha, walikuwa wanavuta kamba, makamishna nikasema toa hapo," alisema.

Alisema Kamishna Jenerali wa Magereza wa sasa amepanda mikorosho, akibainisha kuwa hatua hiyo imemfanya ajiulize "waliokuwapo hawakuona?"

"Mtu anayekupenda anakueleza, ambaye hakupendi hakuelezi. Nina matumaini makubwa mabalozi watatu mlioteuliwa, mtakwenda kufanya kazi, mmepelekwa nchi ambazo ni mkakati ambazo ni Kenya, Msumbiji, Algeria," alisema.

Rais pia alimtaka Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) aliyemwapisha siku hiyo, asiende kustarehe, bali akafanye kazi ili yanayowasumbua wananchi wa kawaida ikiwamo rushwa yakashughulikiwe.

"Nendeni mkafanye kazi kwa sababu kila mmoja alikuwa na nafasi na mkajitathmini mlikosea wapi na mjirekebishe. Nendeni mkachape kazi, hizi ni kazi za watu," alisema.

HABARI KITAIFA

# Watalii waanza kuja Tanzania

Na Augusta Njoji, DODOMA

NDEGE ya kwanza iliyobeba watu saba wakiwamo watalii wanne kutoka Ugiriki ilitua jana katika Uwanja wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA).

Ndege hiyo imewasili zikiwa ni siku chache baada ya kutangaza kufungua kwa anga la Tanzania lililokuwa limefungwa kutokana na ugonjwa wa corona.

Sambamba na hilo, Mei 28, mwaka huu, Tanzania inatarajia kupokea ndege nyingi zaidi ikiwamo za watalii.

Akizungumza jana na waandishi wa habari, Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isack Kamwelwe, alisema ndege hiyo ilitua uwanjani saa tatu asubuhi.

"Ndege iliyotua ilikuwa na watalii wanne na crew ya watu watatu na wametua tayari, wamepokelewa na wamekwenda kuangalia wanyama," alisema.

Aidha, alisema anaratiba ya ndege zitakazofanya safari zake kuja Tanzania na booking zimejaa, huku akisisitiza ifikapo Mei, 28, mwaka huu ndege nyingi zaidi zitatua ikiwamo zilizobeba watalii.

"Yapo mashirika ya ndege yalishajiandaa kama Emirate, Ethiopia, KLM na kwa upande wa zitakazofanya safari za mizigo tulianza na Rwanda Airline kuanza kubeba minofu ya samaki, leo (jana) tumeongeza ndege nyingine Ethiopia Airline ambayo itabeba tani 19 za minofu ya samaki," alisema.

Aidha, waziri huyo alisema Jumapili (Mei 24), ndege ya Ethiopia itarudi tena jijini Mwanza na kubeba tani 40 ya minofu ya samaki.

"Tunaendeleza mazungumzo uwanja wa Mwanza umefunguka na kwa kuwa ni uwanja wa kimataifa, ndege zitaruka kimataifa kwa ajili ya kubeba mizigo na tunaendelea kuongea na Waziri wa Mifugo na Uvuvi na nyama ianze kusafirishwa," alisema.

Katika hatua nyingine, Waziri Kamwelwe alisema Shirika la Ndege (ATCL) linakamilisha taratibu za kuanza kubeba na kupeleka mizigo Ulaya kwa ajili ya biashara.

Aprili, 11, mwaka huu, Mamlaka ya Usafiri wa Anga nchini (TCAA), ilifuta safari zote za ndege za abiria kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa corona.

Hata hivyo, kutokana na tathmini ya mwenendo wa ugonjwa huo, Mei 18, mwaka huu, serikali ilitangaza kufunguliwa kwa usafiri wa anga la Tanzania kwa ndege zote za kibiashara, misaada, kidiplomasia, za dharura na ndege maalum.



Wakazi wa Jiji la Dar es Salaam, wakipata tabu kupanda kwenye mabasi kutokana na kituo cha daladala cha Kawe, jijini humo jana, kuzingirwa na matope. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Diwani kortini shtaka la kupokea rushwa mil. 1/-

Na Hellen Mwango

DIWANI wa Kata ya Kijichi Halmashauri ya Manispaa ya Temeke kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Elias Mtarawanje (29), amefikishwa mahakamani akikabiliwa na mashtaka mawili ikiwamo kushawishi na kupokea rushwa ya Sh. milioni moja kutoka kwa Yusuf Omary.

Mshtakiwa huyo alisomewa mashtaka yake jana katika Mahakama ya Wilaya ya Temeke iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi, Catherine Madili.

Mwendesha Mashtaka wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Mwanakombo Rajabu, alidai kuwa Februari 6, mwaka huu eneo la Mtoni Kijichi, Wilaya ya Temeke, jijini Dar es Salaam mshtakiwa akiwa Diwani wa Kata ya Kijichi, aliomba rushwa ya Sh. milioni moja kutoka kwa Omary kama kishawishi kwake ili asiweze kuzuia malipo ya fidia ya eneo jambo ambalo amelifanya tofauti na uhusiano wa shughuli za mwajiri wake.

Katika shtaka la pili, inadaiwa kuwa Februari 6, mwaka huu, eneo la tukio Mtoni Kijichi mshtakiwa huyo akiwa diwani kwa njia za rushwa alijipatia Sh. milioni moja kama kishawishi kwake ili asiweze kuzuia malipo ya fidia ya eneo, jambo ambalo amelifanya tofauti na uhusiano wa shughuli za mwajiri wake.

Upande wa Jamhuri ulidai kuwa hauna pingamizi la dhamana, upelelezi wa kesi hiyo umekamilika na kuomba mahakama kupanga tarehe ya kumsomea maelezo ya awali.

Akitoa masharti ya dhamana, Hakimu Madili alimtaka mshtakiwa huyo kuwa na wadhamini wawili watakaosaini bondi ya Sh. 500,000, kila mmoja.

Mshtakiwa huyo ametimiza masharti ya dhamana.

Hakimu alisema mahakama yake itasikiliza maelezo ya awali Juni 3, mwaka huu.

# Wabunge wapewa notisi kuhama nyumba za serikali

Na Gwamaka Alipipi, DODOMA

WAKATI Bunge la 11 likitarajiwa kumalizika Juni 19, mwaka huu, imeelezwa kuwa wabunge waliopanga katika nyumba za serikali mjini Dodoma, wameanza kupewa barua za kutakiwa kuondoka.

Mbunge wa Rufiji (CCM), Mohamed Mchengerwa, aliyasema hayo jana bungeni wakati akiomba mwongozo wa spika kuhusu suala hilo, huku akimwomba Spika Job Ndugai, kuzungumza na Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isack Kamwelwe, kuliangalia upya suala hilo na kuwa na subira hadi uchaguzi utakapomalizika.

Mchengerwa alisema asilimia 99 ya wabunge wamepewa barua na Wakala wa Ujenzi Tanzania (TBA), zinazowataka kuondoka haraka katika nyumba za serikali walizokuwa wamepanga.

"Wabunge wengi wameshapewa barua ya kutakiwa kuondoka katika nyumba za serikali na wametakiwa ndani ya muda mfupi wawe wameshaondoka," alisema Mchengerwa na kuongeza:

"Asilimia 99 ya wabunge waliopewa barua hizo ni wa CCM, nikuombe Spika kwa kutambua kazi kubwa wanayoifanya wabunge. Na kutambua shughuli za kibunge zipo Dodoma na Dodoma ndiyo makao makuu ya nchi, nikuombe Spika umuombe Waziri wa Ujenzi atusaidie, iwapo serikali wanataka kutekeleza agizo hili wasubiri hadi uchaguzi mkuu utakapomalizika ndipo wabunge wapatiwe barua hizo," alisema Mchengerwa.

Mchengerwa alisema wabunge walioingia katika nyumba hizo walizikuta chakavu na nyingine mbovu, hivyo walitumia fedha nyingi kuzikarabati.

Alisema wabunge wengine walitumia Sh. milioni tano hadi 10, hivyo Waziri wa Ujenzi anapaswa kulizingatia suala hilo.

Mchengerwa alisema TBA inapaswa kusubiri hadi uchaguzi mkuu ufanyike, na kwamba kwa wabunge watakaopata nafasi ya kuchaguliwa tena wapewe nafasi ya kuendelea kukaa katika nyumba hizo.

**WAZIRI ATOA UFAFANUZI**

Waziri Kamwelwe akijibu hoja hiyo alikiri kuwapo kwa utolewaji wa barua kwa wabunge waliopanga nyumba za serikali wakitakiwa kuondoka haraka.

"Wapo wabunge walioingia mikataba na TBA kwa makubalinao kwamba Bunge ndilo litakuwa linawalipia kodi, wabunge wengine waliingia mikataba ya kujilipia wenyewe kodi," alisema Kamwelwe na kuongeza:

"Kwa sababu suala hili ni la mikataba, Bunge linaisha mwezi wa sita, wabunge wanaolipiwa na bunge mkataba wao utakuwa umeisha, ndiyo maana TBA wameamua kufanya hivyo. Ila wale ambao wanalipa kodi wenyewe wanaweza kujibu barua hiyo, nikiwamo mimi nimesaini mkataba wa kulipa kodi mwenyewe. Hivyo kama nitapata barua nitawajibu kuwa bado nipo," alisema Kamwele.

**MAELEZO YA SPIKA**

Akilitolea ufafanuzi zaidi suala hilo, Spika Job Ndugai, alisema: "Hapa waziri anamaanisha Dodoma ndiyo makao makuu ya nchi, hivyo wabunge jengeni msipende kupanga. Ila hakutaka kusema tuu, ila ndiyo ujumbe wenyewe."

"Anayetaka kiwanja amuone Waziri wa Tamisemi Seleman Jafo, ukikosa kiwanja mfuate Waziri wa Ardhi, Willium Lukuvi. Sisi tulioingia bungeni mwaka 2000 tulipewa viwanja, nikiwamo mimi, juzi nilienda kukifuatilia nikakuta kimechukuliwa, lakini nimekirudisha," alisema Spika Ndugai.

Spika Ndugai aliwataka wabunge ambao wanauhitaji wa kweli wa viwanja wamuone ili awasaidie.

Alisema: "Wabunge wenzetu wa Uganda hawamalizi ubunge bila ya kuwa na nyumba katika Jiji la Kampala, hata Kenya mbunge hamalizi ubunge bila ya kuwa na nyumba Nairobi."

# Waziri alalamika kutokabidhiwa viwanja alivyonunua Dodoma

**Na Gwamaka Alipipi, DODOMA**

WAZIRI wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isack Kamwelwe, amelalamika bungeni kutokabidhiwa viwanja viwili alivyonunua katika Jiji la Dodoma tangu mwaka 2018.

Amesema amefuatilia kwa muda mrefu viwanja hivyo, ikiwamo kumfuata Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Bilinith Mahenge, na Mkurugenzi wa jiji hilo, Godwin Kunambi bila mafanikio.

Kutokana na kushindwa kuvipata viwanja hivyo, Waziri Kamwelwe alilazimika kumuomba Spika Job Ndugai kumsaidia ili aweze kuvipata, ingawa ameshavilipia.

Waziri Kamwele alilazimika kuyasema hayo baada ya Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maendeleo ya Makazi, Willum Lukuvi, kuwataka wabunge wanaohitaji viwanja kwa ajili ya kujenga makazi au nyumba za biashara wamuone na atawasaidia haraka.

Kwenye maelezo yake, Waziri Lukuvi alisema: "Jiji la Dodoma wamejitahidi sana, tumeuza viwanja 10,000. Hadi hapa ndani (bungeni) Naibu Waziri wangu alikuwa anagawa fomu hapa mwaka juzi, watu wamenunua viwanja viwili, vitatu," alisema na kiuongeza:

"Wenye mawazo ya kujenga 'Guest House' (nyumba za wageni), apartments, nyumba za biashara. Hata anayetaka kiwanja aende Jiji, akikosa anione mimi, kuna viwanja vya kumwaga. Hapa ndiyo mahali pake, kwa viongozi kama nyie wabunge hapa ndiyo 'second home'," alisema Lukuvi.

Baada ya maelezo hayo ya Waziri Lukuvi, ndipo Waziri Kamwelwe alipoinuka na kusema:

"Mimi nilipewa ofa nikalipia viwanja viwili siku hiyo hiyo, shahidi yangu Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Mavunde, mpaka leo sijapata kiwanja. Tena mimi ni waziri, nimeongea kwa Mkuu wa Mkoa, kwa Mkurugenzi, hadi leo sijapata kiwanja, nimelipa fedha zote," alisema.

Spika Ndugai ilimlazimu kumweleza Waziri Kamwelwe kuwa atamsaidia kuhakikisha anapata viwanja hivyo.



Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, Brigedia Jenerali mstaafu Emannuel Maganga (kulia), akipokea misaada ya kibinadamu kutoka kwa Mratibu wa Shirika la Msalaba Mwekundu Mkoa wa Kigoma, Khalid Selemani (wa nne kulia) na Mwenyekiti Mussa Kipfumu (wa tatu kulia), kwa ajili ya kusaidia waathirika wa mafuriko katika Wilaya ya Uvinza. **PICHA: PENDO THOMAS**

# Mafuriko yaharibu nyumba 300, wakazi wakosa makazi

**Na Pendo Thomas, KIGOMA**

BAADHI ya wakazi wa Wilaya ya Uvinza mkoani Kigoma hawana makazi kutokana na nyumba 311 kubomoka na zingine kujaa maji kufuatia mafuriko yaliyotokea wilayani humo mwishoni mwa Aprili, hivyo kusababisha kaya hizo kuhifadhiwa na majirani hadi sasa.

Hayo yalibainishwa na Mkuu wa Wilaya ya Uvinza, Mwanamvua Mrindoko, wakati Chama cha Msalaba Mwekundu Mkoa wa Kigoma kilipokuwa kikikabidhi misaada ya kibinadamu kwa waathirika wa mafuriko hayo.

Alisema kaya hizo zimepoteza makazi na kwamba kuna uwezekano wa kukabiliwa na upungufu wa chakula.

Mafuriko hayo yaliyokumba kata sita za wilaya hiyo yameharibu zaidi ya hekari 400 za mazao shambani na vyakula vilivyo hifadhiwa nyumbani pamoja na mifugo kusombwa na maji, hivyo kuomba wadau wengine kuendelea kujitokeza kutoa misaada ya kibinadamu.

Naye Mwenyekiti wa Tanzania Redcross society mkoa wa Kigoma, Mussa Kipfumu, alikitaka chama hicho kupitia wanachama wake kujitolea na kushirikiana na serikali katika majukumu yote ya kibinadamu maafa yanapotokea.

Chama hicho kilikabidhi magodoro 100, blanketi 200, dumu 100, ndoo 100 vyenye thamani ya shilingi 9,273,200.

Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, Brigedia Jenerali mstaafu Emannuel Maganga, aliwataka wananchi kufuata maelekezo wanayopewa na serikali katika ujenzi wa makazi kwani baadhi yao wamekumbwa na mafuriko hayo kutokana na kujenga karibu na mito.

"Wengine mnajitakia, mnayafuata maji...kwa wale ambao kwa hiari yao wameyafuata maji kuwasaidia ni kwa huruma tu za kibinadamu, wewe ukiyafuata maji hilo la kwako," alisema.

Mkazi wa Kijiji cha Kirando, Malilo Ezekiel, alisema mafuriko hayo yamesababisha nyumba zake mbili kubomoka, na kwamba yeye na familia yake wamelazimika kuishi kwa ndugu.

Alieleza kuwa mazao yaliyokuwa shambani yakisubiri kuvunwa pia yaliharibika.

"Hali ni mbaya kwa sasa, tunaishi kwa shida, tunaomba serikali ifanye utaratibu wa kutuwezesha namna ya kupata makazi, vikiwamo vifaa mbalimbali vitakavyowezesha kujenga nyumba za kujihifadhi," alisema.

# Abiria Dar walalamika daladala kukatisha ruti

**Na Maulid Mmabaga**

ABIRIA wanaofanya safari kutoa Segerea kwenda Makumbusho, jijini Dar es Salaam, wamelalamikia baadhi ya madereva wa daladala zinazofanya ruti ya njia hiyo kukatisha safari wakati wa asubuhi kinyume na sheria.

Hali hiyo ilibainika baada ya abiria katika kituo cha Segerea jana kulalamikia baadhi ya daladala kuvuruga utaratibu na kusababisha usumbufu kwa watumiaji wa magari hayo.

Jafari Haule, mkazi wa Segerea alisema utaratibu huo wa baadhi ya madereva unasababisha kuwapo kwa mkusanyiko mkubwa katika vituo vya daladala na kuhatarisha usalama wa kiafya wakati huu wa kupambana na ugonjwa wa Covid -19.

"Baadhi ya daladala zinakuja lakini zinageuzia nje ya kituo, zingine zinaingia, lakini hazichukui abiria, kwa zile zinazo chukua utakuta wanasema wanaishia Ubungo wakifika huko wanatangaza tena kuwa wanaenda Makumbusho," alisema.

Lilian Martin, mkazi wa Segerea alisema hali hiyo inafanyika kwa wiki ya tatu sasa na kugeuka mazoea kwa baadhi ya madereva wakishirikiana na makondakta.

"Tunawaomba maofisa wa usalama barabarani kutusaidia kutatua changamoto hiyo na kuwachukulia hatua ya kisheria watakao wabaini kutekeleza jambo hilo kwa kuwa linasababisha usumbufu mkubwa kwa wananchi," alisema.

Jonassi Lyaheja, ambaye ni miongoni mwa dereva wa daladala zinazolalamikiwa alipoulizwa kuhusu shutuma hizo, alisema kutokana na agizo la 'level seat' vituoni abiria wanapanda na kugeuza na magari.

"Unakuta gari inajaa hata kabla ya kufika mwisho sasa huwezi kuchoma mafuta bila sababu ukizingatia hata kipato chetu cha sasa kimeshuka, ndio maana wakati mwingine tunageuza," alisema.

Nipashe ilipowasiliana kwa njia ya simu na Kamishna Msaidizi wa Polisi Ilala (ASP), Zuberi Phembera, kuhusu tatizo hilo, alisema atalifuatilia jambo hilo kwa kushirikiana na maofisa wa usalama wa barabarani.

"Sikuwa na taarifa ya suala hilo kabla, lakini nitalifuatilia kwa kushirikiana na maofisa wa usalama wa barabarani," alisema.

TANGAZO

# FARM AFRICA

## PUBLICATION OF FINANCIAL STATEMENTS

In accordance with Non-Government Organisations (Amendment) Regulation, 2019. Farm Africa is pleased to publish its financial statements and funding status for the period ended **31 December 2019.**

### STATEMENT OF INCOME AND EXPENDITURE FOR THE YEAR ENDED 31 DECEMBER 2019

| Income | 2019 TZS | 2018 TZS |
|---|---|---|
| Receipts from Donors and Trust | **4,122,689,861** | 5,719,961,109 |
| Other Income | **498,733,125** | 470,440,930 |
| **Total Income** | **4,621,422,986** | 6,190,402,039 |
| **Expenditure** | | |
| Capital Expenditure | **23,044,450** | 1,386,500 |
| Staff Costs | **1,551,428,265** | 1,407,285,470 |
| Support Costs | **226,248,600** | 50,284,767 |
| Support to local partners | **135,408,571** | 3,025,078,529 |
| Training | **495,339,922** | 202,466,890 |
| Programme Development | **188,193,232** | 26,963,290 |
| Marketing and Advertising | **21,287,091** | 11,534,333 |
| Monitoring and Supervision | **513,723,249** | 609,990,645 |
| Dissemination | **17,692,217** | 212,660,908 |
| Project Running | **490,039,964** | 421,615,673 |
| **Total Expenditure** | **3,662,405,561** | 5,969,267,005 |
| **Operating surplus for the year** | **959,017,425** | 221,135,034 |

### STATEMENT OF FINANCIAL POSITION AS AT 31 DECEMBER 2019

| | 2019 TZS | 2018 TZS |
|---|---|---|
| **ASSETS** | | |
| **Current assets** | | |
| Debtors and Accrued Income | **780,222,895** | 1,483,911,098 |
| Bank and Cash | **594,736,400** | 795,545,573 |
| **TOTAL ASSETS** | **1,374,959,295** | **2,279,456,671** |
| **LIABILITIES** | | |
| **Current liabilities** | | |
| Creditors | **855,182,722** | 2,718,697,523 |
| | **855,182,722** | 2,718,697,523 |
| **NET ASSETS/(LIABILITIES)** | **519,776,573** | **(439,240,852)** |
| **GRANT FUND** | | |
| At 1 January | **(439,240,852)** | (660,375,886) |
| | **959,017,425** | 221,135,034 |
| **At 31 December** | **519,776,573** | **(439,240,852)** |

### Funding Analysis for the year ended 31 December 2019

| | Country Office | Sunflower Project | NORAD DECIDE | WFP SORGHUM | USAID/DIA MORINGA | Grand Total |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **EXPENDITURE** | | | | | | |
| Capital expenditure | | 9,324,100 | 13,720,350 | | | 23,044,450 |
| Dissemination | | 14,468,957 | | 3,223,260 | | 17,692,217 |
| Monitoring and Supervision | 3,841,017 | 205,697,048 | 102,314,784 | 201,870,400 | | 513,723,249 |
| Programme Development | 13,728,578 | | 43,051,004 | 126,496,500 | 4,917,150 | 188,193,232 |
| Project Running | 156,987,739 | 188,707,753 | 24,909,065 | 83,472,399 | 35,963,008 | 490,039,964 |
| Staff costs | 413,689,842 | 393,556,317 | 385,674,437 | 282,057,216 | 76,450,453 | 1,551,428,265 |
| Support costs | | 41,974,667 | 179,302,452 | 4,330,081 | 641,400 | 226,248,600 |
| Training | | 301,355,867 | 50,414,004 | 138,569,600 | 5,000,450 | 495,339,921 |
| Support to local partners | | 127,518,571 | 5,520,000 | 2,370,000 | | 135,408,571 |
| Marketing and Advertising | | 19,022,691 | | | 2,264,400 | 21,287,091 |
| | ***588,247,176*** | ***1,301,625,971*** | ***804,906,096*** | ***842,389,456*** | ***125,236,861*** | ***3,662,405,560*** |
| ***INCOME*** | | | | | | |
| Recharges | 494,038,206 | | | | | 494,038,206 |
| Other Income | 4,694,918 | | | | | 4,694,918 |
| AMDT | | 1,432,100,024 | | | | 1,432,100,024 |
| NORAD | | | 766,731,681 | | | 766,731,681 |
| WFP | | | | 823,246,022 | | 823,246,022 |
| USAID/DIA | | | | | 13,297,182 | 13,297,182 |
| Previous Deferred Income | 1,087,314,952 | | | | | 1,087,314,952 |
| **B: Total Funding** | **1,586,048,076** | **1,432,100,024** | **766,731,681** | **823,246,022** | **13,297,182** | **4,621,422,985** |
| **Surplus/(Deficit)** | **997,800,900** | **130,474,053** | **(38,174,415)** | **(19,143,434)** | **(111,939,679)** | **959,017,425** |

The financial statements were authorised for issue and signed by the Management of Farm Africa on 15 April 2020

Tanzania Country Office:
Amverton Tower, Plot no. 1127 2nd Floor
Chole road-Msasani Peninsular
P.O Box 105181,
Dar Es Salaam, Tanzania

E infotanzania@farmafrica.org
W: www.farmafrica.org
T: 255 222 927 802

157488

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Bravo JPM, Kenyatta kuingilia kati mipaka

**MARAIS** John Magufuli wa Tanzania na Uhuru Kenyatta wa Kenya, wamesafisha hali ya hewa, kufuatia hali ya sintofahamu kwenye mipaka ya nchi hizo mbili.

Hali hiyo ilijitokeza hivi karibuni kutokana na kasoro zilizojitokeza kuhusiana na utaratibu wa kuwaruhusu madereva wa malori ya mafuta.

Kikubwa ni utaratibu wa kuwataka wapimwe kupimo cha virusi vya corona, lakini ikaonekana kuna dosari ambazo zilizua shaka kuwa huenda kuna nia mbaya ya kuzorotesha uhusiano mzuri na wa kuhistoria ambao ni wa muda mrefu kati ya mataifa haya jirani ya Afrika Mashariki.

Kwa kuliona tatizo hilo, wakuu hao wawili wa mataifa hayo, wamewaagiza mawaziri wanaohusika na uchukuzi na wakuu wa mikoa iliyoko katika pande zote za mpaka wa Tanzania na Kenya, kukutana na kutatua mgogoro uliosababisha kuzuiwa kwa malori ya mizigo kuvuka mpaka huo.

Rais Magufuli alisema hayo juzi, alipokuwa akiwasalimu wananchi wa Singida akiwa safarini kutoka Chato mkoani Geita kwenda makao makuu ya nchi jijini Dodoma.

Siku chache zilizopita umeibuka mgogoro katika vituo vya mpaka wa Tanzania na Kenya katika Mikoa ya Mara, Mwanza, Arusha na Kilimanjaro baada ya malori ya mizigo ya kutoka Tanzania kuzuiwa kuingia Kenya kwa madai ya madereva wanaopimwa kukutwa na maambukizo ya virusi vya corona.

Rais Magufuli alibainisha kwamba, Rais Kenyatta alimpigia simu Jumanne na Jumatano, na katika mazungumzo yao wamekubaliana kuwa viongozi wa pande zote mbili wanapaswa kukutana na kutatua mgogoro huo haraka iwezekanavyo ili Watanzania na Wakenya waendelee kufanya biashara zao kama kawaida.

Alisema kwamba kuzuiwa kwa malori ya Tanzania yanayokwenda Kenya ama kuzuiwa kwa malori ya Kenya kuja Tanzania hakukubaliki.

Aliwataka viongozi wa pande zote mbili waweke maslahi ya Tanzania na Kenya mbele, waache kuamua mambo kwa jazba na akaagiza wakuu wa mikoa ya Mara, Mwanza, Arusha na Kilimanjaro, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano na Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Kanali Wilbert Ibuge, kuhakikisha mazungumzo hayo yanafanyika ndani ya wiki moja.

Kenya na Tanzania ni nchi ambazo ni wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), ambayo inaziwezesha nchi zote wanachama zikiwamo Uganda, Rwanda, Burundi na Sudan Kusini kushirikiana katika sekta mbalimbali kama za biashara, uchumi, utalii, miundombinu na usafirishaji, kwa kutaja baadhi.

Kwa hiyo njia pekee ya kutatua changamoto zinapojitokeza ni kwa wahusika kutumia njia za mawasiliano na majadiliano ili kuweka mambo sawa kwa manufaa na ustawi wa wananchi wa jumuiya hiyo.


Tunawapongeza wakuu hao wa nchi hizo kuingilia kati kwa kutoa maelekezo kwa mawaziri na maofisa wa kila upande kukutana kwa ajili ya kurekebisha mambo.

Suala hilo linapaswa kuwa fundisho kwa viongozi na maofisa wa serikali za nchi hizo na zingine za EAC kujenga utamaduni wa kukutana na kujadiliana namna ya kumaliza changamoto zinapojitokeza kabla hazijasababisha athari zaidi kwa wananchi na nchi hizo kwa ujumla. Mawaziri, watendaji na maofisa wengine ni wajibu wao kushughulikia na kumaliza changamoto hizo badala ya kuwaachia jukumu hilo wakuu wa nchi na serikali, ambao wana majukumu mengi na makubwa.

Ni matarajio yetu kwamba mawaziri, watendaji na maofisa wetu pia watachukua hatua kushughulikia changamoto zilizoko katika mpaka wa Tunduma, ambapo madereva kutoka nchini wanalalamikia upande wa Zambia kwa kuwanyanyasa, hivyo kutishia kuvuka na malori yao ya mizigo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Itapendeza 'level seat' kwenye daladala ikiwa ya kudumu



Na Sabato Kasika

TANGU Mamlaka ya Udhibiti wa Usafirishaji Ardhini (Latra) kuviagiza vyombo vya usafiri kubeba abiria kulingana na idadi ya viti (level seat), karibu daladala za jijini Dar es Salaam, zimetelekeza maagizo hayo.

Ubebaji huo wa abiria kwa 'level seat' umesukumwa na kuwapo tishio la maambukizo ya virusi vya corona, ambalo liliifanya Latra kusimamia utaratibu huo ambao upo lakini umekuwa hautekelezwi.

Ingawa mwanzoni kulikuwapo na changamoto za hapa na pale, hasa baadhi ya makondakta kutozingatia ubebaji huo wa abiria ambao kimsingi ni wa kisheria, lakini kwa sasa angalau wameanza kuelewa na kuutumia.

Changamoto hizo zilitokana na ukweli kwamba walizoea kujaza abiria kupita kiasi kwa lengo la kujipatia fedha nyingi, lakini sasa hilo halipo wakati huu ambao dunia inakabiliwa na tishio la ugonjwa huo.

Sasa, kwa vile karibu wote wametekeleza maelekezo ya Latra, basi kuna haja mamlaka hiyo kuendelea kusimamia maelekezo hayo hata pale corona itakapokwisha, ili 'level seat' iwe ni ya kudumu.

Ninasema hivyo, kwa sababu kwa tabia ya baadhi ya Watanzania kutoheshimu sheria, inawezekana corona ikiasha na wakarudia kujaza abiria katika magari kupita kiasi kama zamani.

Kwa kuwa sasa wahusika wanazingatia umuhimu wa kubeba abiria kwa idadi inayotakiwa, ni vyema Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani na Latra, wakaendelea kusimamia utaratibu huo hata kama corona itaisha.

Siyo siri kwamba, tangu kurejeshwa 'level seat', siku hizi daladala hazikawii vituoni kusubiri abiria kama ilivyokuwa siku za nyuma na watu wanawahi safari zao.

Imewezekana kuwaweka sawa makondakta hadi wakakubali kubeba abiria kulingana na idadi ya viti, kwa nini utaratibu huo usiendelee hata kama maambukizo ya corona yataisha?

Nadhani 'level seat' isiwe mkakati wa kupambana na kuenea kwa virusi vya corona, pia ni wa kuheshimu sheria usalama barabarani, ambazo zimekuwa zikivunjwa na daladala.

Ilikuwa kawaida daladala kujaza abiria kupita kiasi, kutofunga mlango wakati gari likiwa kwenda mwendo, makondakta kutowapa abiria tiketi na matendo mengine mengi ambayo ni kinyume.

Hilo la kubeba abiria kulingana na idadi ya viti, laweza kuwa limefanikiwa kwa kiasi kikubwa ingawa pia inawezekana wapo baadhi ya makondakta ambao bado kwa kificho hawajali 'level seat'.

Suala la msingi ni kwamba, ubebaji abiria wa sasa katika daladala uwe mfumo wa kudumu, kwa sababu ndivyo sheria za usalama barabarani zinavyotaka, kwamba abiria wasijae katika gari kupita kiasi.

Pamoja na hayo, kuna haja makondakta na madereva kuelimishwa ili watambue na kuzingatia sheria hizo, wasione kama wanaonewa, kwani wapo baadhi yao wanalalamikia 'level seat' kuwa inawaumiza.

Kwamba hawapati fedha nyingi kama zamani walivyokuwa wakijaza abiria kupita kiasi kana kwamba ni halali kufanya hivyo, na kumbe wanakwenda kinyume na sheria kwani haziruhusu ubebaji wa aina hiyo.

Hivyo, waelimishwe, pia Latra na polisi trafiki wasilegeze kamba kwenye hili suala la 'level seat' ili wahusika waache kufanya kazi kwa mazoea bali wafuate sheria zinazowataka kubeba abiria kwa 'level seat'.

Kusiwapo kisingizio chochote cha kusababisha kurudi nyuma na badala yake sheria ichukue nafasi yake katika kusimamia usafiri ili makondakta na madereva wasijifanyie wanavyotaka.

Ikumbukwe, pamoja na kuwapo foleni za magari jijini Dar es Salaam, nyingine zilikuwa zikisababishwa na uzembe wao, kwa kusimama hata pasipo kituo kusubiri abiria hata kama daladala imejaa.

Wao wanaamini kwamba daladala haijai bali ndoo ya maji ndiyo inayojaa, hivyo wana haki ya kuendelea kujaza abiria wanavyotaka, hali ambayo ilikuwa inasababisha watu kuchelewa katika shughuli zao.

Itapendeza, iwapo mamlaka husika hazitawarudisha tena abiria kwenye mtindo huu wa zamani ambao ni kero na tayari wameshanza kuusahau baada ya Latra kusimamia sheria.

# Operesheni kamata watoto yakusanya 119 mitaani

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

KATIKA kupambana na virusi vya ugonjwa wa Covid-19 kwa watoto hasa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari wilayani Kahama, kitengo cha Ustawi wa Jamii, Halmashauri ya mji wa Kahama kimewakamata watoto 119 na kuwaunganisha na familia zao.

Akizungumza jana na gazeti hili, Ofisa Ustawi wa Jamii, Halmashauri ya mji wa Kahama, Abrahamani Nuru, alisema, operesheni hiyo ilikuwa ni kuondoa watoto wanaoishi na kufanyakazi mitaani.

Alisema, walikuwa wamelenga kuanzia umri wa miaka 13 hadi 17 na walifanikiwa kuwakamata watoto 119 na kuwaunganisha na familia zao na wengi wao walikuwa ni wanafunzi wa shule za msingi na sekondari.

"Tulifanya operesheni ya ukamataji wa watoto wa mitaani kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, lengo lilikuwa kuondoa wanaoishi na kufanyakazi mitaani na watoto wengi walikuwa ni wanafunzi wa shule za msingi na sekondari kutoka Kahama na nje ya wilaya," alisema Nuru.

"Operesheni hii tulianza Machi 28, mwaka huu na kumaliza Aprili 3 na jumla ya watoto 119 wenye umri chini ya miaka 18 tuliwakamata na kuwaunganisha na familia zao na mpaka sasa hakuna mtoto mwenye umri huu yuko mitaani anafanyakazi," alisema.

Nuru aliwataka wazazi na walezi kutoawaacha watoto kuendelea kurandaranda mitaani au kuwahusisha katika shughuli za biashara ndogondogo kwa kipindi hiki cha kujikinga na Covid-19.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, wakati akipokea msaada wa chakula kwa ajili ya wananchi waliopata maafa kutoka Shirika la Redcross alisema, kwa sasa wamefanikiwa kuwaondoa watoto wote mitaani na kuwarejesha majumbani mwao.



Wakazi wa Jiji la Dar es Salaam, wakipita kwenye maji yaliyotuama katika eneo la Feri, kutokana na mvua iliyonyesha juzi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Kaya 5,000 wasiojiweza kunufaika misaada

**Na Mary Geofrey**

KAYA 5,000 za watu wasiyojiweza, wenye ulemavu, yatima na wajane, zinatarajia kunufaika na misaada ya chakula kutoka taasisi ya Nama kupitia washirika wake, Annahl Trust na Nice Tanzania.

Misaada hiyo yenye thamani ya Sh. milioni 800 itatolewa kwa wakazi wa Dar es Salaam, Pwani na Visiwani Zanzibar kwa lengo la kuunga juhudi za serikali katika janga na ugonjwa wa Covid-19.

Mratibu wa misaada hiyo wa taasisi ya Nama, Hamza Jabir, aliwaeleza waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam kuwa misaada hiyo itajumuisha pia vifaa tiba vyenye thamani ya Sh. milioni 500.

"Taasisi hizi zimeamua kushirikiana kuunga mkono juhudi za serikali katika kupambana na maambukizo ya corona kwa Watanzania hivyo tutatoa msaada wa Sh. bilioni 1.3 unaojumuisha vifaa tiba na chakula kwa familia zisizojiweza," alisema Jabir.

Alibainisha misaada ya chakula watakayotoa kuwa ni mchele kilo 10, unga kilo 10, sukari, mafuta, vitakasa mikono na barakoa kwa kila familia yenye uhitaji.

Kuhusu vifaa tiba, alisema watatoa mavazi ya kujikinga ya watoa huduma PPE, Oxymeter, oxygen concentrator, Thermoscanner, vitanda vya chumba cha uangalizi maalum (ICU) na vingine vinavyohitajika kwa mwongozo wa serikali na Wizara ya Afya.

"Utekelezaji wa utoaji misaada hii utaanza Mei 27, na kuendelea na kwa mtaa wa mwananyamala pekee tutazifikia kaya 200 na tutashirikiana na viongozi wa jamii na serikali hasa katika kuzitambua kaya zinazolengwa katika maeneo yote," alisema Jabir.

Naye Mratibu mwenza wa shughuli hiyo, Seleman Abdallah, aliishukuru serikali kwa kuendelea kuwapa ushirikiano.

"Tunaishukuru taasisi ya Nama Foundation kwa kutambua juhudi za serikali na washirika wake An-Nahl na Nice Tanzania, ambalo ni wadau wakubwa katika kusaidia jamii, tuendelee kuunga mkono serikali na kupongeza kwa juhudi zake kuisadia na kufikia jamii kubwa ya Watanzania itakapopata uwezo zaidi," alisema Abdallah.

# W'biashara waliokopa NMB wapewa unafuu

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB Plc imetangaza unafuu wa ulipaji mikopo kwa wateja wa biashara ndogo na za kati (SME/MSME) na wakubwa ili kuwasaidia kukabiliana na madhara yaliyotokana na janga la Covid - 19 kwenye biashara zao.

Hatua hiyo ni jitihada ya benki katika kutoa ahueni kwa wateja wake hususani sekta zilizoathiriwa zaidi na janga hilo.

Takribani wateja 412 wa biashara ndogo na za kati wameshapata ahueni hii kwa kupitia likizo ya marejesho ya mikopo yao na wengine wakiongezewa muda wa kulipa mikopo hiyo ili kuwasaidia kukabiliana na madhara yaliyoletwa na Covid – 19 katika biashara zao.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa NMB, Ruth Zaipuna, alisema jana kuwa athari ambazo zimetokana na janga la Covid-19 kwa watu wa kawaida na wafanyabiashara zimekuwa si kubwa sana ukilinganisha na nchi ambazo zilifunga shughuli zote na watu kujifungia ndani.

Alisema hata hivyo, uamuzi wa nchi nyingine kujifungia umeleta mtikisiko katika biashara duniani na hivyo kuathiri baadhi ya wateja wa benki hiyo nchini.

"Kama Benki, tunatambua kuwa huu ni wakati mgumu kwa wateja wetu ambao biashara zao zimeathirika kutokana na mtikisiko huu kutoka nje... tumedhamiria kutoa ahueni kutokana na mahitaji ya wateja na ukubwa wa athari, hii ni kwa sababu si biashara zote na wateja wote wameathirika kwa kiwango sawa, mkazo ni katika biashara zilizoathirika zaidi na Covid-19," aliongeza.

"Tunapenda kuwahakikishia wateja wetu kuwa hawako peke yao kwenye safari hii. Milango yetu ipo wazi na tupo tayari kuwasaidia katika nyakati hizi zisizo na uhakika za janga la Covid-19. Mara zote lengo letu ni kuhakikisha ukuaji wa uchumi wa nchi yetu. Njia pekee tunayoweza kufanya hilo ni kuhakikisha kuwa ukuaji wa wateja wetu ni endelevu, hivyo umuhimu wa kuwapunguzia mzigo huu katika kipindi hiki."

"Pamoja na ahueni hii ya kifedha, pia tutatoa mafunzo ya kibiashara na nasaha mbalimbali za uwekezaji na usimamizi wa fedha kwa njia za kielektroniki kwa kutumia wataalamu wa ndani," alisema Zaipuna.

# Waziri Mwakyembe ataka wanahabari wapewe taarifa

**Na Eleuteri Mangi, DODOMA**

WIZARA ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo imezitaka ofisi za umma kutoa taarifa kwa wanahabari kwa kuwa ni takwa la kisheria kwa mujibu wa Katiba.

Waziri mwenye dhamana ya habari, Dk. Harrison Mwakyembe, alisema hayo alipokutana na ujumbe wa viongozi wa Chama cha Waandishi wa Habari kutoka mkoani Arusha pamoja na Asasi ya Vyombo vya Habari Mbadala (Alternative Media), jana jijini Dodoma.

"Serikali haina ugomvi na vyombo vya habari, bila vyombo vya habari hatutaweza kuwahabarisha wananchi masuala mbalimbali ya maendeleo ya nchi yetu," alisema. Aliwakumbusha wanahabari kuwa kazi wanayofanya ni muhimu na nchi zilizoendelea bado zinatumia vyombo vyao vya habari ikiwamo Shirika la Utangazaji la Uingereza (BBC) ambalo lina miaka zaidi ya 90 na linatangaza habari zake kwa lugha zaidi ya 40, ili kuwafikia wananchi wake na dunia kwa ujumla.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Chama cha Waandishi wa Habari kutoka Mkoa wa Arusha, Claud Gwandu, amemshukuru Dk. Mwakyembe kwa mapokezi, majadiliano yenye tija kwa uwazi na ukweli na kumpongeza kwa kazi nzuri anayofanya katika sekta anazozisimamia.

"Tunamshukuru waziri kwa kutupa nafasi ili tuweze kushirikiana katika kuimarisha tasnia ya habari iwe bora kwa mustakabali wa nchi yetu," alisema Gwandu.




Baadhi ya wafanyakazi wa Benki ya Exim Tanzania wakiongozwa na Mkuu wa Idara ya Masoko na Mawasiliano wa benki hiyo, Stanley Kafu (kushoto), wakikabidhi msaada wa vyakula na vifaa kinga dhidi ya maambukuzo ya virusi vya corona kwa walezi wa kituo cha kulelea watoto yatima cha Malaika Kids wilayani Kinondoni jijini Dar es Salaam, jana.**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Exim yawezesha yatima mikoa 4

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Exim na wafanyakazi wa benki hiyo, wamekabidhi msaada wa vyakula na vifaa kinga dhidi ya maambukuzo ya virusi vya corona kwa vituo vinne vya kulelea yatima na watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu katika mikoa ya Dar es Salaam, Zanzibar, Mtwara na Tanga.

Uwezeshaji huo uliofanyika jana, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa Uwajibikaji kwa Jamii (CSR) unaotekelezwa na benki hiyo unaofahamika kwa jina "Exim Cares", na lengo ni kuwawezesha watoto hao waweze kufurahia Sikukuu ya Eid-Ul-Fitr kama watoto wengine waliopo majumbani mwao, huku pia wakijilinda dhidi ya maambukizo ya corona.

Kwa upande wa Jiji la Dar es Salaam makabidhiano yaliongozwa na Mkuu wa Idara ya Masoko na Mawasiliano wa benki hiyo, Stanley Kafu, ambapo akiwa kwenye kituo cha kulelea watoto yatima cha Malaika Kids, kilichopo wilayani Kinondoni, aliwasisitiza watoto wanaoishi kwenye vituo hivyo kusoma kwa badii kwa kuwa taifa linategemea mchango wao katika kufanikisha maendeleo.

Msaada huo ulihusisha vyakula vya aina mbalimbali ikiwamo mchele, mafuta ya kupikia, sukari, maharage, vinywaji pamoja vifaa kinga dhidi ya virusi vya corona.

"Zikiwa zimesalia siku chache tu kabla ya kusherehekea Sikukuu ya Eid Ul Fitr, Benki ya Exim tuliona ni vema tusherehekee pamoja na watoto yatima pamoja na wale wanaoishi kwenye mazingira magumu kwa kuwapatia mahitaji haya muhimu ili na wao waweze kufurahia siku hiyo, muhimu kama wenzao waliopo majumbani...tunashukuru wametupokea vizuri na wameonyesha kufurahishwa na hilo," alisema.

Akizungumza baada ya kupokea msaada huo, mlezi wa kituo hicho, Neema Mohamed, aliishukuru benki hiyo kwa wema huo huku akitoa wito kwa taasisi nyingine pamoja na watu binafsi kujitokeza pia ili kusaidia watoto wanaoishi kwenye vituo hivyo kwa kuwa mahitaji bado ni makubwa.

# Wataalamu wa uvuvi kupata ajira kimataifa

**Na Gwamaka Alipipi, DODOMA**

WATAALAMU wa vyombo vya uvuvi nchini wataanza kuajiriwa kitaifa na kimataifa, baada ya Bunge kuridhia mkataba wa kimataifa wa viwango vya mafunzo na utoaji vyeti kwa wafanyakazi wa vyombo vya uvuvi wa mwaka 1995.

Akisoma mkataba huo bungeni jijini hapa jana, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, alisema kuridhiwa kwa mkataba huo kutaleta manufaa tisa kwa taifa.

Dk. Kalemani alisema kwanza utatoa fursa za ajira za ndani na za kimataifa kwa wataalamu wa vyombo vya uvuvi.

Alisema pia kutahakikisha kuwapo kwa ukaguzi wa waangalizi wenye weledi ambao kuwapo kwao kutahakikisha matumizi endelevu ya rasilimali za bahari.

"Kutaimarisha vyuo vya ndani vya mafunzo ya uvuvi na kutambulika kimataifa, kuwapo kwa viwango bora vya ufundishaji wa wanafunzi katika vyuo vya uvuvi nchini," alisema Waziri Kalemani.

Alisema kuidhinishwa kwa mkataba huo kutaimarisha usalama wa wafanyakazi katika vyombo vya uvuvi na hivyo kupunguza ajali.

"Kwa mujibu wa takwimu za mwaka 1994, kazi ya uvuvi ilionekana kuwa ni kati ya kazi hatari duniani kwa kusababisha wastani wa wavuvi 24,000 kupoteza maisha kila mwaka. Idadi hii ni zaidi ya mara 10 ya vifo vinavyotokea katika meli za biashara," alisema Waziri Kalemani.

Alisema mkataba huo pia utawezesha kuimarika kwa ulinzi, usalama na uhifadhi wa mazingira ya bahari pamoja na kuimarisha kwa upatikanaji wa takwimu na taarifa mbalimbali katika sekta ya uvuvi.

Alisema manufaa ya kupitishwa kwa azimio hilo ni pamoja na kuwezesha Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi kutoa mafunzo na vyeti vinavyotambulika kimataifa katika uvuvi wa vyombo vya bahari kuu.

Waziri Kalemani alisema baadhi ya madhara yanayoweza kutokea iwapo mkataba huo hautaridhiwa ni pamoja na Watanzania kutoajirika katika nafasi za kimataifa eneo la uvuvi wa bahari kuu, kinyume na wale wanaofanya kazi katika meli za biashara.

Alisema pia Tanzania itakosa nguvu za ukaguzi na uangalizi wenye weledi kwa meli za kimataifa zinazofanya kazi katika bahari kuu kwa ajili ya kuhakikisha matumizi endelevu ya rasilimali za bahari.

Alisema kutasababisha kukosekana kwa usimamizi wa ulinzi, usalama na uchafuzi wa mazingira ya bahari, Tanzania kutoonekana kuwa eneo salama la kuvua samaki kwa kutofikia viwango vya kimataifa.

Alisema Tanzania itakosa mapato kutokana na kukosekana kwa ajira za Watanzania katika soko la kimataifa.

Akisoma ushauri wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, Makamu Mwenyekiti wa kamati hiyo, Hawa Mchafu, alisema ni muhimu kwa serikali kuzingatia mikataba ambayo ni mizuri na yenye faida kwa nchi na kuiwasilisha bungeni ili kuridhiwa mapema na kuanza kunufaika badala ya kusubiri athari zitokee.

Alisema ni muhimu serikali iharakishe kuandaa sera ya bahari kwa kuwa ni muhimu hasa kama nchi inataka kuwekeza na kunufaika na uchumi unaotokana na bahari.

Vilevile alishauri Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC), kuimarishwa na kuboreshwa kwa kuhakikisha linakuwa na vitendea kazi bora na vyenye kukidhi viwango vya Taifa na kimataifa kwenye kufanya ukaguzi.

# RC ataka wananchi kuendelea na maisha

**Na Joctan Ngelly, KIGOMA**

MKUU wa Mkoa wa Kigoma, Emmanuel Maganga, amewataka wananchi wa mkoa huo kuendelea na maisha yao kama kawaida na kuwasikiliza wataalamu wa afya kwa kuvaa barakoa na kunawa maji tiririka.

Maganga alitoa rai hiyo jana wakati akizungumza na wadau mbalimbali wa mkoa huo, baada ya kupokea misaada ya vifaa vya kujikinga na ugonjwa wa corona pamoja na michango ya fedha kutoka kwa wadau hao jana eneo la Mnarani, Manispaa ya Kigoma/Ujiji.

Aliwataja wadau waliotoa msaada huo kuwa ni Sido, Adventure Connection, Kiwanda cha maji cha Tanganyika, Mamboleo Pharmacy, Turashashe Pharmacy, Kivuma Investment, Unicef, WHO na UNHCR.

Aliwataka wadau hao waendelee kutoa misaada kwa sababu ugonjwa huo utaendelea kuwapo hadi Mwenyezi Mungu atakapoamua kuuondoa.

Aliwataka waratibu wa misaada na michango kusimamia vizuri ili ilenge kwa watu wasio na uwezo, wazee, vijijini na wakimbizi.

Maganga alisema kwa hali wanayokwenda nayo ni nzuri hadi sasa Mkoa wa Kigoma una mgonjwa mmoja wa corona ambaye hali yake ni nzuri na anatarajiwa kuruhusiwa wiki ijayo.

Alisema jana kama walivyoagizwa na serikali waliwaondoa watu wote 60 kwenye karantini na wote walikuwa wametoka nchi za nje na watarudia kwenye utaratibu wa kawaida kwa wale watakaoonyesha dalili watawaweka kwenye maeneo maalumu.

Aliwataka wananchi wa mkoa huo kuendelea na maisha yao ya kawaida isipokuwa wawasikilize wataalamu pamoja na kuvaa barakoa, kunawa maji tiririka kama walivyoanza mwanzo.

Kwa upande wake mtaalamu wa kushughulikia magonjwa ya mlipuko wa Shirika la Afya Duniani (WHO), Dk. Jairos Hiliza, alisema kazi yake kwa niaba ya shirika hilo ni kuangalia milipuko inavyo endelea katika nchi hususan Mkoa wa Kigoma.

Dk. Hiliza alisema shirika hilo limechangia Tanzania Sh. milioni 330 ambazo asilimia 70 ya fedha hizo tayari zipo kwa ajili ya mkoa kuendelea kuzitumia.



Baadhi ya waandishi wa habari mkoani Iringa wakipata maelezo kutoka kwa mmoja ya wawekezaji wa elimu mkoani humo, Jesca Msambatavangu (aliyeketi), kuhusu elimu kwa njia ya mtandao unaojulikana kama "Corona Season Schools" kwa wanafunzi wa shule za awali, msingi na sekondari ili wanafunzi waendelee na masomo, mjini Iringa jana. **PICHA: FRIDAY SIMBAYA**

## Kicheko wanakijiji kupata umeme Rea

**Na Zuena Msuya, TABORA**

WAKAZI wa Kijiji cha Loya wilayani Uyui mkoani Tabora, wameishukuru serikali kupitia Wizara ya Nishati kwa kuwaunganisha na kuwawashia umeme katika kijiji hicho waliokuwa wakiona kama ndoto.

Walieleza hayo baada ya Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, kuwasha umeme katika kijiji hicho na kukagua maendeleo ya usambazaji, juzi.

Walisema, miaka mingi walikuwa wakipewa ahadi zisizotekelezeka na wakati mwingine wakikatishwa tamaa ya kupata umeme kwa kuwa kijiji hicho kiko umbali mrefu kutoka ilipo miundombinu ya umeme na jiografia isiyo rafiki kufika maeneo hayo.

"Huyu waziri ameandika historia hapa Loya, haijawahi kutokea kiongozi mkubwa ngazi ya waziri kufika katika kijiji chetu tangu kimeanzishwa, wengi wanakuja katika wilaya hii, lakini wanaishia huko mijini tu, vijijini hawafiki," alisema mwanakijiji Josephat Wamalulu.

Dk. Kalemani kwa upande wake alisema baada ya kusikia malalamiko na kuona uhitaji mkubwa wa umeme kwa kijiji hicho ambacho hakijafikiwa na mradi wa kusambaza umeme (REA) kwa kipindi hiki, aliliagiza Shirika la Umeme nchini (Tanesco) kupeleka umeme kwa gharama zao katika kijiji hicho.

Alisema kijiji cha Loya kina wakulima wengi wa mpunga, karanga na wafanyabiashara ambao wanahitaji huduma ya umeme katika kuendesha shughuli zao za kiuchumi.

Tanesco ilitenga zaidi ya Sh. bilioni tatu ili kuhakikisha umeme unafika katika kijiji hicho, ambacho kiko umbali mrefu kutoka ilipopita miundombinu ya umeme.

"Niliwaagiza Tanesco kuleta umeme hapa Loya, kama mlivyoona ina wakazi wengi wakulima na wafanyabiashara ambao wanahitaji umeme katika shughuli zao," alisema.

Vile vile, Tanesco iliagizwa kuendelea kusambaza na kuwasha umeme kwa wakazi wa eneo hilo waliokwisha kulipia gharama za kuunganishiwa umeme ndani ya siku saba baada ya kulipia.

Aliwataka wakazi wa Loya kutumia umeme huo kujiendeleza kiuchumi badala ya kuutumia kuwasha taa peke yake.

Mbunge wa Jimbo la Igalula, Musa Ntimizi, aliwataka wafanyabiashara katika kijiji hicho kutanua wigo wa kibiashara na wakulima wa mpunga kuongeza thamani ya mazao yao ili kupata faida zaidi.

# Shivyawata yaomba wadau nakala vitabu nukta nundu

**Na Enock Charles**

SHIRIKISHO la Vyama vya Watu wenye Ulemavu Tanzania (Shivyawata), limewaomba wadau kuendelea kuwachangia kupata nakala za vitabu vya nukta nundu.

Pia wameomba kupatiwa vifaa vingine vya kuwawezesha kupata elimu na kupambana na maambukizo ya virusi vya corona.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Mwenyekiti wa Shivyawata, Ummy Nderiananga, alisema makundi takribani kumi ya walemavu ambao wanakadiriwa kufikia milioni tatu nchi, wana mahitaji mbalimbali yanayohitaji msaada wa wadau hasa katika kipindi hiki cha vita dhidi ya corona, vikiwamo vitabu hivyo, ambavyo vinatoa elimu kuhusu ugonjwa huo.

"Nawaomba watu mbalimbali waendelee kutusaidia watu wenye ulemavu hususan kupata vifaa vya kunawia na 'material' mbalimbali ambazo inatakiwa watu wenye ulemavu wawe nazo ili kujikinga kama barakoa na vitakasa mikono," alisema Nderiananga.

Naye Mratibu wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC), Onesmo Ole Ngurumwa, akikabidhi nakala 1,500 za vitabu vya nukta nundu, alisema watu wenye ulemavu hawapaswi kusahaulika katika mapambano dhidi ya corona kwa kuwezeshwa kwa vifaa mbalimbali.

"Hawa watu wenye ulemavu wanahitaji vitu kama hivi kwa sababu hawawezi kusoma vitabu vya kawaida, tunaposema makundi yote yafikiwe ndiyo vitu kama hivi... ukimpa vitabu vya kawaida hawezi kusoma, ila ukimpa kama hivi anasoma kama 'document' za kawaida."

Kwa mujibu wa Nderiananga, kundi la watu wasioona lina walemavu wanaokadiriwa kufikia 25,000, na vitabu vilivyotolewa havijakidhi mahitaji, na kuomba msaada zaidi wa wadau kwa kuwa vipeperushi vinavyochapishwa kwa maandishi ya kawaida pamoja na nakala za video haviwezi kuwafikia.

# Bunge laelezwa Acacia ilivyonunuliwa na Barrick

Na Augusta Njoji, DODOMA

BUNGE limeelezwa kuwa kampuni ya Acacia ilikwishanunuliwa na Kampuni ya Barrick ambapo mgodi wa North Mara kwa sasa unamilikiwa kwa ubia na serikali kupitia Kampuni ya Twiga.

Hayo yalielezwa bungeni jana na Wizara ya Madini ilipokuwa ikijibu swali la Mbunge wa Serengeti (CCM), Marwa Chacha.

Katika swali lake, mbunge huyo alisema Serengeti ni moja ya wilaya zinazoathirika na uwepo wa mgodi wa Acacia ambao umepakana na vijiji vya Borenga, Nyiboko na Marasomoche.

"Je, serikali ipo tayari kuwataka Acacia kutoa Social Corporate Responsibility (CSR) kwa vijiji hivyo pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti?" Alihoji.

Katika majibu ya wizara hiyo, ilisema kifungu cha 105 (1) na (2) cha Sheria ya Madini Sura ya 123, kinamtaka mmiliki wa leseni, kuandaa mpango wenye tija wa mwaka wa wajibu wa kampuni kwa jamii uliokubalika kwa pamoja na Mamlaka ya Serikali ya Mtaa husika au Mamlaka ya Serikali za Mtaa kwa kushauriana na Waziri anayehusika na Mamlaka za Serikali Mitaa na Waziri anayehusika na Fedha.

"Mgodi wa North Mara wamekuwa wakitimiza wajibu wao kwa kuandaa na kupeleka Mpango wa CSR katika Halmashauri ya Wilaya ya Tarime kwa mujibu wa Sheria ya Madini Sura ya 123," ilisema.

Ilieleza kwa mwaka 2019, mgodi uliandaa mpango wa utoaji huduma wenye kiasi cha Sh. bilioni 5.75 na kupitishwa na Halmashauri ya Tarime kwa ajili ya vijiji 11 katika miundombinu ya elimu, afya, barabara na maji ambavyo ni vipaumbele vya Halmashauri ya Tarime.

"Kwa kuwa masuala ya CSR yanasimamiwa na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) wakishirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango, hivyo basi, Wizara ya Madini itawasiliana na Tamisemi kuhusu pendekezo la kuwezesha vijiji vya Borenga, Nyiboko na Marasomoche pamoja na Wilaya ya Serengeti kunufaika na CSR inayotolewa na Kampuni ya Barrick Co.Ltd," ilisema.



# Bei ya mahindi mwaka huu yatajwa

SERIKALI imesema bei za mahindi kwa mwaka huu sokoni zimeanzia Sh. 500 mpaka Sh. 800 kwa kilo moja ya mahindi.

Hayo yalibainishwa jana na Wizara ya Kilimo ilipokuwa ikijibu swali la Mbunge wa Kwela (CCM), Ignas Malocha.

Katika swali lake, mbunge huyo alisema serikali kupitia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) imeshusha bei ya kununua mahindi toka bei ya kilo moja kwa Sh.500 mpaka Sh.380 kwa kilo.

"Je, ni sababu zipi zimepelekea serikali kupunguza bei ya mahindi badala ya kuongeza na je, serikali inaweza kuwaelekeza wakulima gharama ya kuzalisha kilo moja ya mahindi toka kuandaa shamba, kulima, kupanda, kuvuna mpaka kufikisha sokoni?" Alihoji.

Katika majibu ya wizara hiyo ilisema bei ya mazao hupangwa na nguvu ya soko na serikali kupitia wakala haijashusha bei ya mahindi.

"Bei zimekuwa zikibadilika kwa kuzingatia bei za soko wakati wa ununuzi wa mahindi, ambapo katika msimu wa ununuzi 2019/20 wakala umenunua nafaka kwa bei Sh.500 hadi Sh.700 kwa kilo," ilisema.

Aidha, ilisema wakala umekuwa ukilipa ushuru wa mazao kwa mujibu wa Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 1982 kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa unakonunua mazao ya wakulima.

"Gharama ya kuzalisha kilo moja ya mahindi ambazo mkulima anaingia kutokana na kuandaa shamba, kulima, kupanda, kuvuna mpaka kufikisha sokoni hutofautiana kutoka sehemu moja hadi nyingine kutokana na utofauti wa aina ya udongo, kiasi cha pembejeo za kilimo zinazotumika, mbinu za kilimo na tija inayopatikana katika mavuno na uzalishaji," alisema.

Hata hivyo, ilisema kutokana na tofauti ya gharama hizo, si rahisi kuelekeza gharama aina moja kwa wakulima wote.

Ilishauri wakulima kutumia maofisa kilimo au maofisa ugani wanaopatikana katika mikoa na halmashauri zao ili kubaini gharama halisi za uzalishaji kwa eneo husika.

Kadhalika, ilisema kwa sasa NFRA imeongezewa jukumu jipya la kufanya biashara ya nafaka kwa kununua na kuuza kwa faida.

Aidha, ilisema kwa kuzingatia msingi huo wa biashara NFRA ina wajibu wa kununua kwa kuzingatia bei ya soko ya kununulia na kuuzia mazao yake ili wakala usipate hasara na kupoteza fedha za umma.

"Hivyo, kupanda na kushuka kwa bei ya mahindi inategemea nguvu ya soko kwa kuzingatia mahitaji na ugavi na sio serikali kupanga bei hizo," ilisema.



## Mbunge ahoji ongezeko la bajeti Tarura

MBUNGE wa Masasi (CCM), Dk. Rashid Chuachua, amehoji mpango wa serikali wa kuongeza bajeti ya Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (Tarura) katika Mji wa Masasi, mkoani Mtwara.

Akiuliza swali bungeni jana, Dk. Chuachua alisema Mji wa Masasi unakua kwa kasi licha ya kutengewa kiasi cha Sh. milioni 700 kwa ajili ya miundombinu kupitia Tarura.

"Je, serikali ina mpango gani wa kuongeza bajeti hiyo?" Alihoji.

Katika majibu ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), ilisema bajeti ya matengenezo ya barabara katika Halmashauri ya Mji wa Masasi imeongezeka kutoka Sh. milioni 686.1 katika mwaka wa fedha 2018/19 hadi Sh. milioni 860 kwa mwaka wa fedha 2019/20.

"Azma ya serikali ni kuendelea kuongeza bajeti kadri makusanyo ya mapato ya serikali yanavyoongezeka ili kukidhi matengenezo ya mtandao wa barabara za Mamlaka za Serikali za Mitaa kupitia Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (Tarura)," ilisema.

**Katika majibu ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), ilisema bajeti ya matengenezo ya barabara katika Halmashauri ya Mji wa Masasi imeongezeka kutoka Sh. milioni 686.1 katika mwaka wa fedha 2018/19 hadi Sh. milioni 860 kwa mwaka wa fedha 2019/20.**





Ukurasa 12

Simulizi ndoa kuvunjika na kulipuka umasikini kifamilia

BUFE

IJUMAA MEI 22, 2020

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



Ukurasa 13

Ijue Saccos iliyokamata walimu na watumishi umma Missenyi, Bukoba

BIASHARA

# Mwenyekiti Mkuranga ang'aka 'amcos' kuamua bei peke yake

• DC: Tunadaiwa Sh. bn. 1 za korosho; Sh. 33 dalili 'kupigwa'

**Na Yasmine Protace,** Mkuranga

JANA jarida la Afya na Mazingira lilikuwa na mwendelezo wa simulizi za Mkuranga, kuhusu afya ya wanafunzi kipindi cha likizo iliyopo.

Ni mwendelezo wa simulizi ya Ijumaa iliyopita kuhusu janga la wakazi kukosa daraja ambalo ni janga la kiuchumi.

Kimsingi, wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani wakazi wake wakuu ni wakulima na zao lao la biashara mahsusi ni 'dhahabu ya taifa' korosho.

Kutokana na zao hilo kuwa juu hivi sasa, wakazi wa Mkuranga, kama walivyo wenzao wa mkoa wa Pwani; Rufiji, Kibiti na Kibaha, pia mikoa ya Lindi na Mtwara, wanawajibika kwa palizi za kila msimu, ili waweze kunufaika na jasho lao shambani.

Vilevile Mkuranga wanajituma kulima mazao mengine kama mihogo, viazi, matikiti maji, nazi na aina mbalimbali ya matunda.

Hiyo yote ni kumuwezesha mwananchi kuinuka kiuchumi na kujiongezea kipato yeye na familia yake.

Hivi karibuni katika Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga, walilalamikia vyama vya msingi vya ushirika maarufu 'amcos' kuwa chanzo cha kudumaza uchumi wa wilaya ambazo kimsingi wakazi wake ni wakulima.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya Mkuranga, Juma Abeid, ambaye ni pia ni Diwani wa Kata ya Magawa, anasema Mkuranga ina jumla ya 'amcos' 45 zinazotambulika.

Abeid anafafanua kuwa, vyama hivyo vinashindwa kufanya mikutano na wakulima, ili kujadili changamoto za korosho.



Sehemu ya korosho ikiwa ghalani Mkuranga, ikifanyiwa ukaguzi na uongozi wa serikali mwaka jana. **PICHA: MTANDAO.**

> **Katika mwaka wa fedha 2017/2018, walikusanya jumla ya Sh. bilioni 6.3; mwaka 2019/2020 walifikisha Sh. bilioni 6.5.**

Mwenyekiti analalamika vyama hivyo vya ushirika vipo chini ya serikali, lakini inashangaza kuyumbisha bei ya wananufaika wakulima, hivyo anacholilia ni 'amcos' zisifanye bei peke yao.

"Amcos zote zinatakiwa kuwa na bei moja," anasema Abeid, huku akilalamika kuwa dai lingine katika kipindi kilichopo, mazao ya wakulima yanaharibika kwa kukosa wanunuzi.

Anafika mbali na malalamiko ya kutokukubaliana na ushuru wa mazao kwa bei Sh. 127 kwa kilo, akihoji kwa gadhabu: "Mkulima atapata wapi huo ushuru, ukizingatia hakufanya biashara kutokana na mvua ambazo zimeharibu korosho na kusababisha kurudishwa majumbani?"

### DC AFAFANUA

Mkuu wa Wilaya hiyo, Filbeto Sanga, katika kikao cha Baraza la Madiwani, anasema korosho za mwaka 2018 na 2019, wakulima wanadai malipo ya mauzo zaidi ya Sh. bilioni moja

Sanga anaahidi malipo kufanyika taratibu na hadi sasa anataja changamoto iliyopo ni kwa baadhi ya viongozi kutokuwa waaminifu katika vyama vya ushirika vya wakulima.

"Kuna chama kimeleta majina ya wakulima wanadai milioni 33. Nimewaambia wawalete hao wanaodai na sio majina, hawajaletwa mpaka leo wanaodai na sisi tutafuatilia. Tukibaini kuna udanganyifu na majina yasipothibitishwa, tunayafuta," anasema Mkuu wa Wilaya.

Sanga anasema licha ya Mkuranga kuwa na jumla ya vyama vya ushirika 45vya wakulima, vilivyofanya mikutano kwa mujibu wa katiba zao, ni vyama 14 tu.

Rai yake ni kwamba wataalamu wa ushirika wanapaswa kwenda kusimamia mikutano ya vyama hivyo.

Kuhusu wabanguaji korosho, Sanga anawakumbusha ubia wa ufanisi wa kazi yao, madiwani wanapaswa kuendelee kushirikiana na wananchi, kukamilisha kazi za wananchi.

Moja ya majukumu yao madiwani, Sanga anakumbhusha ni kuwa karibu na wataalamu wa korosho, ili wajifunze jinsi ya kutatua matatizo ya wakulima wa zao hilo.

### DED NA MAPATO

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya Mkuranga, Injinia Mshamu Munde, anasema makusanyo ya mapato katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/2016, ilikuwa kiasi cha Sh. bilioni 2.5.

Pia, anasema katika mwaka wa fedha 2017/2018, walikusanya jumla ya Sh. bilioni 6.3; mwaka 2019/2020 walifikisha Sh. bilioni 6.5.

Anasema hadi kufikia mwezi uliopita, alitarajia kufika malengo asilimia 100 ya malengo na anajigamba: "Tuna uhakika makusanyo yatapanda mpaka kufikia Sh. bilioni saba,"

UCHUMI

JICHO KUTOKA PEMBA...

# Simulizi ndoa kuvunjika na kulipuka umasikini kifamilia

• Ya simanzi mama hadi mtoto na faraja uchokonozi wa Tamwa

**NA Mwandishi Wetu,** PEMBA

WAKATI serikali, wadau na wanaharakati wako katika vita vya haki za watoto kuondosha unyanyasaji, bado kuna mikasa ya aina hiyo inaendelea.

Mikataba kimataifa, kikanda na kitaifa inaelekeza wajibu wa kila mmoja kuwalinda watoto dhidi ya maovu na haja ya kuwapa huduma stahiki kama elimu, chakula, lishe bora na kuimarishwa kiafya.

Wajibu wa kumlinda mtoto kupitia serikalini na mashirika yasiyo ya serikali, yanatunga sera, sheria na miongozo ya utekelezaji na wawajibikaji wakuu ni wazazi na hasa wanandoa.

Uchunguzi wa Nipashe kisiwani hapa, umebaini bado kuna tatizo kubwa la unyanyasaji wa mtoto.



Kinamama wakazi wa Shehia za Majenzi na Shumba wilayani Micheweni, Pemba walipokuwa katika mkutano unaowahusu. **PICHA: MAKTABA**

### VIONGOZI SERIKALI

Mratibu wa Wanawake na Watoto wa Shehia ya Mjiniole, Pemba anasema wazazi wanapotengana, watoto wanakumbwa na mengi, ikiwamo kubakwa, mimba na ndoa za umri mdogo zinazowakosesha maendeleo.

Anasimulia mwaka jana alipokea kesi ya mama wa watoto wawili waliotelekezwa na mume tangu ujauzito wa mtoto wa pili mpaka umri wa miaka mitatu sasa.

"Wote ni watoto wa kiume, wa kwanza amefikia miaka tisa hajapelekwa skuli, linaloumiza zaidi nimegundua ameshaanza kufanyiwa ulawiti," anasema.

Pia, ana simulizi ya mama wa watoto tisa, kati yao watano hawasomi; huku kesi nyingine ya namna hiyo, familia yenye watoto wanne wote hawajaenda shule.

"Kesi hizi zipo nyingi sana, lakini hawaripoti, isipokuwa mwaka jana nilipokea kesi tano," anaeleza.

Ofisa Wanawake na Watoto Wilaya ya Wete, Siti Suleiman Juma, ana ufafanuzi: "Asilimia kubwa ya watoto wanaojishughulisha na ajira ni wanaoishi na mzazi mmoja, hivyo huathirika kisaikolojia kutokana na kukumbana na kadhia mbalimbali katika jamii.

"Inapotokezea baba 'kamtalaki' mama, basi awashughulikie watoto, unapowadharau watoto na wao watakudharau, kwani itakuwa umechangia kudumaza maendeleo yao, mama pekee hawezi kumudu majukumu yote."

Siti ana mtazamo kwamba, changamoto za kinamama katika kesi hizo, wengi hasa wasiokuwa kazini hawajui mahali pa kupashughulikia.

Ofisa Ustawi wa Jamii Wilaya ya Wete, Haroub Suleiman Hemed, ana lake: "Watoto wanaoishi na mzazi mmoja huduma zinakuwa ni tofauti na yule anayeishi na wazazi wawili, hukosa uwezo wa kujieleza kwa umakini, hukosa fursa, pia hukosa ukaribu wa wazee."

> **"Kuna tatizo, sheria inazungumzia idadi ya pesa kuwa isizidi robo ya mshahara, hivyo kutokana na mshahara ulivyo mdogo hautoshelezi hasa kwa mama mwenye watoto wasiopungua wanne.**

Anawashauri wanandoa kuwa wavumilivu katika misuguano na inapobidi, watumie taratibu rasmi kama za kidini kusuluhishana, ili kudumisha malezi yenye maadili.

"Kuna mama wa Kipangani Wete ameachwa na watoto kwa zaidi ya miaka saba, baba wa watoto amehamia Tanga, hivyo mtoto wake alitaka kujitundika baada ya kukerana na mtoto mwenzake (jirani) kutokana na kumkebehi kwa maisha wanayoishi," anasimulia.

Ofisa Ustawi wa Jamii huyo ana takwimu za kati ya Januari na Novemba mwaka jana, Wete ilipokea kesi 85 za kudai matunzo ya watoto, baada ya wazazi kuachana au kutelekezana na kati yake 69 zimepatiwa ufumbuzi, saba zilikuwa zinaendelea kushughulikiwa.

Pia, mwaka 2018 ofisi hiyo ilipokea mashauri 34 ya mivutano ya kimalezi na kesi 71 za kutelekezwa. Naibu Mrajis wa Mahakama Kuu Pemba, Abdul-razzak Abdulkadir Ali, anakiri kupokea kesi za baba wanaotelekeza watoto katika Mahakama ya Kadhi.

Sheikh Mohamed Ali Hamad, Kadhi wa Mahakama ya Wilaya Wete, anasema ni adimu wanawake walioachwa kufika mahakamani, badala yake hufika waliopo kwenye ndoa, amama wakidai huduma au kulalamikia kutelekezwa.

Anatoa mfano, mwaka juzi, zilipokewa kesi tisa za watoto kukosa matunzo na mwaka jana 15, kati yake 11 zilipatiwa maamuzi.

### WAATHIRIKA WAFUNGUKA

Nafhat Salim Yahya, mkazi wa Limbani, Wete Kaskazini, anasisitiza kutengana wazazi kunaathiri maendeleo ya watoto kwa mahitaji muhimu, kama afya na elimu kwa ujumla.

"Mtoto aliyesoma anaweza kuajiriwa au kujiajiri mwenyewe kutokana na fani anayosomea na akili yake inafikiria maendeleo zaidi, lakini ambaye hakusoma akili yake inadumaa," anafafanua Nafhat.

Hamad Ali Abdallah, mkazi wa Shehia ya Shengejuu, Wete, ana maelezo kwamba wazazi wanapoachana, maisha duni hasa kwa watoto huchukua nafasi.

Mkazi wa Shehia ya Mjiniole (29), aliyeachika akiwa na mtoto na ujauzito, anasimulia kukosa huduma ya baba wa watoto kwa zaidi ya miaka minne, hali iliyomkwamisha mtoto kuhudhuria masomo.

"Baba yao ni mwajiriwa wa serikali na nilimshtaki mahakamani ili angalau anipe pesa nimpeleke skuli, lakini hakutekeleza amri ya mahakama na kila akiitwa hafiki," anaeleza.

Mama anaeleza kwa masikitiko ana mume mwingine sasa, ila shida kuu katika maisha mapya ni umaskini wa mume kumhudumia.

Mama wa miaka 46 mkazi wa Shehia hiyo, ana simulizi: "Siku zote walipokuwa wakirudi skuli, zaidi ya maji ya kunywa hawakuti kitu kingine humu ndani, hivyo walichoka hali hii na wakaniambia liwalo na liwe kuanzia leo hatuendi shule.

"Hatujui tunachokisoma, ni njaa tu kutwa na tukirudi hamna chakula. Bora tukusaidie kulima tupate angalau cha kutia tumboni."

Mama kijana wa miaka 20 mkazi wa Wete, anaelezea maswahibu yaliyomfika kifamilia, baada ya wazazi kuachana akiwa na miaka 13, wao watoto walisambaratika hadi leo, huku wengine wakikabiliwa na matendo mbaya.

Anasimulia wanavyokabili maisha, ni kuranda vichakani na Pwani kuokota vinavyolika, hali iliyozaa dosari mdogo wake kubakwa.

"Kuna tatizo, sheria inazungumzia idadi ya pesa kuwa isizidi robo ya mshahara, hivyo kutokana na mshahara ulivyo mdogo hautoshelezi hasa kwa mama mwenye watoto wasiopungua wane," anafafanua.

### TAMWA & WADAU

Mratibu wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (Tamwa) Pemba, Fat-hiya Mussa Said, anasema wamekuwa wakiwatetea kinamama na watoto, kuhakikisha wanaishi salama.

"Sisi Tamwa tunashirikiana na waandishi wa habari kuibua vitendo vya udhalilishaji, ikiwamo la kukoseshwa huduma, ili kinamama wahamasike kwenda kwenye vyombo vya sheria kudai haki zao," anaeleza.

Anasema, baada ya kesi hiyo ya watoto waliotelekezwa kuibuliwa na wanahabari, walijitokeza wafadhili kuwapatia chakula cha kujikimu, sambamba na kuwatengenezea makazi ya muda.

Mratibu wa Jumuiya ya Tumaini Jipya Pemba (TUJIPE), Tatu Abdalla Mselem, ana ufafanuzi: "Mtoto ndiye anayekumbwa na athari za talaka kwani anakosa huduma zote alizokuwa azipate akiwa na wazazi wawili, lakini ile fimbo inaendelea kumpiga mtoto kwa kukosa huduma muhimu...ukizingatia mama atakayeachiwa ulezi hana huduma."

Mkataba wa Kimataifa wa Kulinda Haki za Mtoto wa Novemba 30 mwaka 1989, uliotiwa saini na nchi 197 duniani ikiwamo Tanzania, unaeleza haki za watoto, kijamii, kisiasa na kiuchumi, kupinga udhalilishaji na utumikishwaji watoto.

Aidha, kuna nyenzo kama hiyo, Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto, uliopitishwa na Umoja wa Afrika (AU) mwaka 1990.

UCHUMI

# Ijue Saccos iliyokamata walimu na watumishi Missenyi, Bukoba

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

• Kusamehe deni 'waliotumbuliwa' vyeti • Mwasisi wake asimulia ilichomfanyia • Yasaidia madawati 200, kila wilaya yapata 100




Mkuu wa Wilaya ya Missenyi, Kanali Denice Mwila (kushoto na shati la kitenge), akipokea madawati 100 kutoka Burute Saccos. Kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi, Innocent Mkandara. **PICHA: LILIAN LUGAKINGIRA**

KATIKA aina za ushirika zilizomea nchini, ule wa kuweka na kukopa, maarufu Saccos, kwa sasa umekamata sana nchini.

Mkoani Kagera katika wilaya za Bukoba na Missenyi, mwaka 2006, walianzisha Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo cha Walimu na Watumishi wa kada nyingine, kitwacho Burute Saccos Ltd, kikiwa imara kwa miaka 14 sasa.

Ni chama ambacho hadi kufikia Desemba 31 mwaka jana, kilishatoa mikopo kwa wanachama wake, zaidi ya shilingi bilioni 2.2.

Hata hivyo, ni ripoti inayoonyesha baadhi ya wanachama walishindwa kurejesha mikopo yao, hivyo kusababisha deni la zaidi ya shilingi milioni 97.2 ambayo haijalipwa. Hadi kumalizika mwaka jana, Burute Saccos ilikuwa na jumla ya wanachama 1,351 na mtaji wa zaidi ya Sh. bilioni 1.9, kwa mujibu wa hesabu zake zilizokaguliwa.

### MWENYEKITI

Gerald Kigundu, Mwenyekiti wa Burute Saccos anasema walilazimika kuingia mkataba na kampuni maalumu ya kukusanya madeni, kuhakikisha deni linarejeshwa kwa wakati.

Kwa mujibu wa mkataba uliosainiwa baina ya pande zote mbili, kuna wanachama 37 wanaodaiwa kiasi hicho hadi kufikia Machi 31 mwaka huu.

Mwenyekiti huyo anasema, chama kilianza na wanachama 520 wakiwa na mtaji wa zaidi ya shilingi milioni 34.5 uliojumuisha hisa za wanachama (Sh. milioni 22.4); Akiba ya lazima Sh. milioni 2.4; akiba za mafungu Sh. milioni 1.8; tengo la mikopo iliyoshakani Sh. milioni 1.8 na malimbikizo ya ziada zaidi ya Sh. milioni 6.1.

Kwa mujibu wa Kigundu, waanzilishi wa Burute Saccos walikuwa walimu pekee na baadaye ikafungua milango kwa watumishi wa umma kada nyinginezo, lengo ni kuwapunguzia adha ya kukopa benki kwa riba kubwa.

"Wakati chama kinaanzishwa kilikuwa kinatoa mikopo kwa riba ya asilimia 18, lakini kwa sasa kinawakopesha wanachama kwa riba ya asilimia tisa tu kwa mwaka," anasema.

"Kama chama tuna jukumu la kuendelea kutoa mikopo kwa wanachama wetu, kusimamia na kuratibu urejeshaji wa mikopo, kukusanya akiba, hisa na amana kutoka kwa wanachama, ili kuwezesha umoja wetu kuwa endelevu," anasema.

Pia, anaeleza sababu ya kuanzisha usahirika huo ilikuwa kuwanusuru wanachama wake walioanza kukopa pasipostahili kwa riba kubwa.

"Hiki ni chombo cha heshima ambacho kinatunza pia faragha za wahusika, baadhi yao heshima zilianza kushuka kutokana na mikopo isiyostahili," anasema Kigundu, anayeeleza hatua za awali, chama hakikuwa na mtaji unaotosheleza mahitaji.

Kigundu anataja jitihada za kujiboresha walizozifanya ni kuwahimiza wanachama kuongeza uwekezaji katika hisa, akiba na amana.

"Mbali na mikopo kila mwisho wa mwaka tunatoa gawio, pia tunatoa elimu kwa wanachama ikiwamo ya ushirika na ujasiriamali, ili wajue matumizi bora ya mikopo. Pia, tunafanya tathmini kwa mikopo tunayotoa ili kuona maendeleo ya mtu aliyekopeshwa," anasema.

Kwa mujibu wa mwenyekiti, kazi ya kuhakiki vyeti kwa watumishi wa umma iliyofanywa na serikali mwaka 2016, iliwapoteza wanachama 24 walioondolewa kazini wakiwa na mikopo yenye zaidi ya Sh. milioni 67.9 kufikia Desemba mwaka jana.

Kuhusu namna inavyowiana na jamii, Kigundu anasema, mwaka huu chama kimetoa msaada wa madawati 200, nusu yake kwa Shule za Msingi Kemondo, Mubembe na Ibaraizibu, zilizoko katika Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba.

"Madawati mengine 100 yametolewa kwa shule tatu za msingi ambazo ni Bugango, Mabale na Mwisa za wilaya ya Missenyi, msaada wote huu una thamani ya shilingi milioni 11," anasema mwenyekiti.

Pia, anasema wamewekeza katika shamba la miti lenye ukubwa wa ekari 1.2, imenunua na kumiliki hisa katika benki mbalimbali; kununua kiwanja na kujenga ofisi yake inayorahisisha huduma na kuboresha mazingira ya kufanyia kazi.

### IENDAKO

Mwenyekiti Kigundu anasema, Burute Saccos ina mipango ya kupunguza kiwango cha riba kwa wanachama, kuwezesha wanufaike, inayoendana na mtazamo wa kuongeza idadi ya wanachama wake.

Ni mkakati unaoendana na kuimarisha mfumo wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehama), ili watendaji husika waweze kutoa mikopo kwa njia ya mtandao (online).

"Kwa sasa anayehama eneo la Saccos ilipo anapoteza uanachama, lakini kwa mpango huu uliopo wa kuimarisha mfumo wa Tehama, utawezesha hata walioko nje ya eneo kunufaika," anasema Kigundu.

Kufuatia chama hicho kuwa na uchaguzi mkuu mwaka huu anatumia fursa hiyo kuwashauri wanachama kuwachagua viongozi wenye weledi ambao wataweza kusimamia na kuendesha chama chao vizuri na kuwezesha kuendelea kuwepo kwa manufaa zaidi kwa wanachama.

### DC MISSENYI

Kanali Denice Mwila, Mkuu wa Wilaya ya Missenyi, ni miongoni mwa viongozi waliopokea msaada wa madawati kwa ajili ya shule tatu za msingi zilizoko wilaya kwake.

Anatumia fursa hiyo, kuishukuru Burute Saccos kuchangia madawati, lengo ni kuboresha mazingira ya watoto kujifunzia. Rai yake ni taasisi nyingine kuiga mfano.

"Shule zilizolengwa kweli zina mahitaji makubwa ya madawati, mfano Bugango, shule ya msingi ina wanafunzi wengi na mahitaji ni makubwa mpaka tumelazimika kuanzisha darasa jingine pembeni, ili kuona kama itaweza kumudu idadi ya wanafunzi waliopo," anasema.

> **"Nilikuwa na kuku kama 200 na sasa baada ya kuona wamezeeka nimewauza na kupata shilingi 900,000, lakini najiandaa kuleta wengine.**

### MWASISI WAKE

Brighton Mwombeki, mwanachama mwanzilishi wa Burute Saccos, anasema mikopo aliyokwishachukua kwa awamu tano, imemsaidia kuboresha maisha yake, amekarabati nyumba yake, kuendesha kilimo na ufugaji.

"Nilikuwa na kuku kama 200 na sasa baada ya kuona wamezeeka nimewauza na kupata shilingi 900,000, lakini najiandaa kuleta wengine.

"Pia, nina ng'ombe, nalima bustani kama nyanya, kabichi, pilipili hoho, nyanya chungu na mabohora (passion fruits)," anasema.

Anataja mengine; mashamba ya migomba, kahawa yenye miche 400 na miti ekari mbili, miradi iliyowezesha kumpatia mahitaji muhimu ya familia yenye watoto wanane, saba wanalipiwa ada na mahitaji ya shule.

Mwombeki, hasiti kuwashauri watumishi wenzake kuchukua mikopo, wakiwa tayari na mipango mizuri ya matumizi yake.

"Kuna watumishi wengine wana kawaida, wakisikia kuna sehemu wanatoa mikopo wanakwenda kuchukua bila kuangalia athari zake, hawajui wataitumia kwa mambo gani na watalipa vipi, matokeo yake mshahara unatoka hela yote inachukuliwa," anasema.

BIASHARA

LIKIZO YA CORONA...

# Kinamama waliohamishia ofisi nyumbani wana simulizi kibao

• Mengi wasiyoyajua, watoto nao ofisi • Mtihani mkuu; kutenga mtoto na kazi



Maisha halisi ya watoto katika 'Likizo ya Corona.' **PICHA: MTANDAO**

**Na Elizabeth Zaya**

MACHI 17 mwaka huu, ndiyo siku serikali ilitangaza kuwapo ugonjwa wa Corona nchini baada ya kuripotiwa kisa cha mgonjwa wa kwanza wa ugonjwa huo.

Miongoni mwa hatua za kwanza zilizochukuliwa na serikali ni pamoja na kufunga kwa muda shule na vyuo vyote ili wanafunzi warudi na kutulia majumbani.

Baadhi ya ofisi pia zilichukua hatua ya kufunga ofisi zao na kulazimia kufanyia kazi nyumbani. Kuna wafanyakazi waliolazimika kufanyia kazi zao majumbani, wanasema wanalazimika kufanya kazi hizo ndani ya tishio la ugonjwa huo wa corona.

Wazazi wanasema, kama ilivyo kawaida ya watoto wengi wanapokuwa na wazazi karibu, hupendelea zaidi wacheze nao hususani wanaokuwa na umri mdogo.

Ni hali inayowapa wakati mgumu kumudu kufanya shughuli zao za kiofisi wakiwa nyumbani.

**MASHUHUDA**

Hannah Mwandoloma, ni miongoni mwa wanaofanya shughuli zao nyumbani katika kipindi cha tahadhari ya ugonjwa Corona.

Anasema yeye ni mama wa watoto watatu, wote wanafunzi walioko nyumbani kwa kipindi ambacho shule zimefungwa na inamlazimu agawane muda na watoto wake.

"Ni changamoto kwa kweli, unapokuwa uko bise na kazi zako, lakini wakati huohuo na watoto nao wanataka mcheze na vituko vingine vingi, kwa hiyo ni changamoto kwa kweli,"anasema Hannah.

> **Ukweli ni kwamba mambo ni magumu, stress zinazidi ila mzazi ni mlezi, tusizembee tufuatilie watoto kwa karibu ili waendelee kujifunza kila siku.**

Pia, anasema kipindi inambidi kufuatilia masomo yao kwa muda mwingi tofauti na ilivyokuwa hapo awali. Anasimulia: "Yaani kipindi hiki ni 'Corona vs parenting and home schooling' (mpaka wa uzazi na shule nyumbani). Mimi nimejifunza kucheki homework (kazi za shule) kila siku.

"Ukweli ni kwamba mambo ni magumu, stress zinazidi ila mzazi ni mlezi, tusizembee tufuatilie watoto kwa karibu ili waendelee kujifunza kila siku."

Mzazi mwingine anayeitwa Ana Ngisyem, anasema si rahisi sana kufanya kazi na kuangalia watoto watoto kwa wakati mmoja. Anasimulia: "Si rahisi sana kufanya kazi na kuangalia watoto, wakati mwingine mwanangu huwa anataka 'attention'(umakini) zaidi umsikilize yeye tu.

Mzazi mwingine aliyejitambulisha kwa jina moja la Alfac, anasema kunawakati kazi zake anafanya kupitia 'video', hivyo akiwa katikati ya mazungumzo, mtoto huingilia kato mazungumzo yake kikazi.

"Kusema kweli nimejifunza uvumilivu. Yaani katikati ya 'call' (simu) mtu ghafla anajipenyeza anadai chapati," anasema na kuongeza kuwa changamoto hizo za watoto zimemsaidia kujifunza mapishi ya aina tofauti kutokana na mahitaji ya watoto wake.

Pia, anasema amezoea kuwasaidia watoto wake kufanya kazi za shule tofauti na ilivyokuwa hapo awali akifafanua: "Ila kutokana na hali hii nimejifunza na kupika, 'homework' nimezoea, maana kila siku lazima niangalie na kwa sasa 'nime -advance' (kupiga hatua) maana nawafundisha kabisa,"anasema Alfacj.

Mama huyo anasema kutokana na majukumu mengi, aliyonayo hivi sasa za kazi za ofisi nyumbani, kusimamia watoto wake kusoma pamoja na kuhakikisha wanapata chakula yeye hajijali tena.

"On top of that (zaidi ya hapo), nimezidi kujisahau, 'time for myself' (muda wangu) umezidi kwisha kabisa," anasema Alfacj, anayesema amebuni ratiba binafsi, baada ya kubanwa na mambo mengi, ili kuhakikisha kila kitu kinafanyika.

"Kwa sasa muda ambao nakuwa bize na kazi na wao pia wanakuwa 'bize' na shule, wanasoma vitabu au kufanya homework, hii ni kuanzia saa tatu asubuhi baada ya chai,"anasema Alfacj.

"Baada ya hapo saa saba mchana tunapumzika kwa ajili ya chakula cha mchana, hapo nawapatia ruhusa ya kucheza wakati mimi namalizia kazi zangu za mchana.

"Ila hata wakati wanaendelea na masomo kabla ya kuanza kucheza huwa nalazimika kuwa nawachungulia mara kwa mara kuona wanafanya nini.

"Ila wakati wa kuwasimamia kwenye 'home work' mara nyingi huwa inanilazimu niwe nao karibu kwa sababu mtoto wangu mmoja ni mdogo sana na anasoma online," anasema.

Anasema kila siku huwa inamlazimu kuamka mapema zaidi ili kuwaandalia watoto wake chai kabla ya kuanza kazi zake.

Penina Malundo, ni mama wa mtoto mmoja, anasema wakati mwingine hulazimika kuacha kufanya kazi zake na kuanza kumbembeleza.

"Kwa kweli kufanya kazi nyumbani ni tofauti na kufanya kazi ukiwa ofisini. Nyumbani hata ujifungie vipi ili watoto wasikuone, lakini ukisikia sauti analia utalazimika tu kutoka ili usikie kimetokea nini na wakati huo itakuchukua muda hata wa nusu au robo saa kumbembeleza," anasema Malundo.

Anaongeza: "Na hiyo ni mojawapo ya changamoto ya kukupotezea 'concentration' (umakini) ya kazi na inaonyesha ni namna) gani ilivyo ngumu kufanyia kazi nyumbani wakati na watoto wapo."

Mama huyo anataja mbinu mbadala, kwamba umakini ni mpaka pale mtoto anapolala usingizi. Anaendelea: "Mimi nyumbani nina msaidizi wa kazi ambaye ndiye pia huwa ananisaidia kulea mtoto.

"Lakini, pamoja na hayo akiwa ananiona huwa anataka akae na mimi muda wote na wakati pekee ambao huwa nafanya kazi vizuri ni pale anapolala usingizi, hapo huwa inabidi nifanye haraka haraka kabla hajaamka.

"Na hii wakati mwingine inachangia usifanye kazi kwa kasi ile ambayo tumezoea ukiwa ofisini. Sisemi kwamba kwa sababu ya kufanyia nyumbani unaweza kuharibu kazi.

"Lakini,. ni kweli kwamba kutokana na harakaharaka za kukimbizana umalize kabla ya mtoto hajaamka wakati inachangia usiifanye kwa ufanisi zaidi."

Anasema, katika kipindi kilichopo, anafanyia kazi zake nyumbani na kupunguza safari zisizo za lazima na amepata muda wa kutosha kufahamu vitu vingi kutoka kwa mtoto wake ambavyo katika kipindi cha nyuma hakuvifahamu.

"Kwa kweli mbali na changamoto ninazoziona za kusumbuliwa na mtoto kwa kufanyia kazi nyumbani, lakini pia kwa sababu sina mizunguko tena, imekuwa kama fursa nzuri pia ya kujifunza mambo mengi kutoka kwa mtoto wangu," anasema Malundo.

"Nimekuwa kama mwalimu wake kwa baadhi ya vitu vingi, pamoja na kwamba mtoto wangu ni mdogo na hajaanza shule bado, lakini tayari nimeanza kumfundisha baadhi ya vitu na nimegundua kwamba ni mwepesi sana wa kuelewa na ni mtundu.

"Nimefahamu kwamba anaelewa sana kujifunza kupitia katuni, kwa hiyo natumia njia hiyo kumfundisha vitu mbalimbali."





## Wasiovaa barakao kushushwa kwenye magari

**Na Peter Mkwavila, DODOMA**

UMOJA wa wafanyabiashara waendao minadani mkoani Dodoma (Uwabimodo), umesema kuwa wafanyabiashara watakao kaidi kuvaa barakoa na kunawa mikono kwa maji na sabuni watashushwa kwenye magari.

Kauli hiyo ilitolewa na Makamu Mwenyekiti wa umoja huo wa wafanyabiashara, Jeremia Magawa, alipokuwa akizungumza na vyombo vya habari kuhusu juhudi wanazozifanya kuhakikisha wanapambana na maambukizo ya virusi vya ugonjwa wa corona.

Alisema kuwa kwa kuzingatia umuhimu wa afya za watu, uongozi umepitisha maazimio kwa pamoja kuwa wafanyabiashara wote watakaobainika kutovaa barakoa hizo na kunawa maji na sabuni watalazimika kushushwa kwenye magari yaendayo minadani.

Pamoja na angalizo hilo, umoja huo kwa kushirikiana na viongozi wa afya katika maeneo husika, wanatoa elimu kwa wateja wao kuwaelimisha kujikinga.

Alisema wamelazimika kufanya hivyo kutokana na kushirikiana na wataalamu wa afya kupewa elimu ya kujikinga na maambukizo ya ugonjwa huo.

Uongozi huo umeamua kutoa elimu kwa jamii wanayoihudumia ikiwa ni pamoja na wao kuwa mstari wa mbele kutimiza masharti ya kujikinga na maambukizo ya corona kwa kufuata masharti ya wataalamu wa afya.

Alisema ili wao wawe kioo katika jamii, uongozi huo umekuwa ukiwahimiza wafanyabiashara wote kuhakikisha wanavaa barakoa, kuwa na vitakasa mikono na kuvitumia muda wote, kunawa maji tiririka na sabuni kabla ya kupanda magari na baada ya kuteremka katika magari.

Pia, umoja huo umepongeza na kushukuru jitihada za Halmashauri ya Jiji la Dodoma kwa kuwawezesha kufanya shughuli zao katika hali ya usalama na mafanikio zaidi tofauti na hapo awali walikuwa wakifanya biashara zao katika mazingira hatarishi kutokana na kutotambulika.

"Kabla hatujawa na umoja huu na hatujatambuliwa rasmi na Jiji tulikuwa tukifanya kazi zetu katika sehemu hatarishi ya barabara ya kumi eneo la Independence na wakati mwingine hata mali zetu zilikuwa zikipotea kwenye mazingira ya kutatanisha," alisema.

Mwenyekiti wa Kamati ya Mipango na Fedha Uwabimido, Gideon Mdumli, alisema kuwa bado wanakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni kukosa eneo maalum ambalo umoja huo unaweza kujenga ofisi zao na kufanya shughuli zao.

Alisema, kwa hivi sasa wamejipanga hivyo wanahitaji kupata ardhi ili wajenge ofisi zao zitakazoambatana na sehemu ya kuhifadhi bidhaa zao ambazo watazipeleka minadani kwa ajili ya kuziuza na kuwahudumia wananchi.

Kwa upande wake, Ofisa Masoko wa Jiji la Dodoma, James Yuna, alisema kwa kushirikiana na Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, wamezungumza na wafanyabiashara hao.

Aliupongeza umoja huo kwa jitihada za kuhakikisha wafanyabiashara wanaepukana na maambukizo ya ugonjwa wa corona kutokana na misimamo waliyojiwekea ya kujilinda na janga hilo.

# Wenye ulemavu kutosikia waomba maeneo biashara

**Na Peter Mkwavila, DODOMA**

WATU wenye ulemavu wa kutosikia mkoani hapa wameiomba Ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, kuwapatia maeneo yatakayowawezesha kufanya shughuli mbalimbali za ujasiriamali na kujiingizia kipato ili kuondokana na utegemezi wa kuomba mitaani.

Ombi hili lilitolewa na Mwenyekiti wa chama hicho, Japhary Gama, alipokuwa akizungumza kwa niaba ya watu wenye ulemavu kutoka Chama cha Michezo cha Viziwi (DODSA), jijini hapa.

Akizungumza kwenye kikao hicho, mwenyekiti huyo ameiomba ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji kuwapatia maeneo ambayo yatawawezesha kufanya shughuli mbalimbali ambazo zitakazowaingizia kipato, na hatimaye kuachana na dhana iliyojengeka ya kuonekana kuwa wao hawana uwezo wa kufanya kazi.

Gama, alisema kuwa kwa upande wao watu wenye ulemavu walio wengi wana uwezo wa kufanya shughuli mbalimbali za ujasiriamali, changamoto waliyonayo ni kupata maeneo ambayo kwa upande wa jiji ndiyo wenye mamlaka ya kuwapatia.

"Wengi wetu hapa kati ya hawa wanachama wa chama cha michezo cha viziwi, wanauwezo wa kufanya kazi na wakaweza kujitegemea kupitia kipato watakachokipata, hivyo tukiwezeshwa tunaweza kuondokana na dhana ya kutegemea wahisani," alisema Gama.

Kwa upande wake ofisa masoko wa jiji hilo la Dodoma James Yuna, aliwataka watu hao wenye ulemavu wa kutosikia kuunda vikundi vya pamoja ili waweze kuwezeshwa na hatimaye wapatiwe maeneo ambayo yanayoweza kujipatia kipato kupitia fursa walizokuwanazo.

Yuna alisema ili watatuliwe changamoto walizo nazo kwa urahisi zaidi wanatakiwa kuungana kwa pamoja na kutoa kero zao ili waweze kusikilizwa na hatimaye kupatiwa maeneo.

"Kwa umoja wao walionao ofisi ya mkurugenzi inaweza kuwatatulia kero hiyo badala ya changamoto zao zikaletwa kwa mtu mmoja mmoja, fursa zipo ambao wao wanaweza wakapatiwa na kuwawezesha kufanya kazi ambazo zinazoweza kuwaingizia kipato bila kutegemea wahisani ukizingatia kuwa uwezo mnao wa kufanya kazi," alisema Yuna.

Katika hatua nyingine ofisa huyo aliwataka watu hao wenye ulemavu kuendelea kujizatiti katika kujilinda na maambukizo ya ugonjwa wa corona kwa vitendo kulingana na hali waliyonayo.



Watoa huduma za afya ngazi ya jamii, wilayani Chemba, mkoani Dodoma, wakiwa kwenye baiskeli zao, baada ya kukabidhiwa msaada na Taasisi ya Mkapa juzi, kwa ajili ya kuwarahisishia utendaji kazi. Watoa huduma kutoka vijiji 79, walinufaika. **PICHA PAUL MABEJA**

# Bei ya sukari bado tatizo wanaouza rejareja

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

LICHA ya serikali kufanikiwa kuwadhibiti wafanyabiashara wakubwa wa sukari katika uuzaji wa bidhaa hiyo, bado kumekuwa na changamoto kwa wafanyabiashara wa rejareja kutekeleza bei elekezi kwa Mkoa wa Dodoma ya Sh. 2,900 kwa kilo.

Bei ya sukari kwa wafanyabiashara wa rejareja kilo moja wanauza kwa Sh. 3,000 tofauti na bei iyotangazwa na serikali kuwa katika mkoa wa Dodoma wananchi wauziwe kwa Sh. 2,900.

Mmoja wa wasambazaji wa sukari mkoani hapa Salman Gullamal, akizungumza jijini hapa jana, alisema hakuna sababu ya wafanyabiashara wa sukari kuuza bidhaa hiyo zaidi ya bei elekezi kwa kuwa wamewapunguzia bei ya bidhaa hiyo.

Alisema mfuko wa kilo 50, za sukari anauza Sh. 130,000 kutoka bei ya awali ya Sh. 137,000, alisema kwa mfanyabiashara wa rejareja ana uwezo wa kuuza kilo moja Sh. 2,700 na akapata faida.

"Nashindwa kuelezwa shida ni nini hadi bei ya sukari bado inakuwa kubwa kwa wauzaji wa rejareja ambao wanawahudumia wananchi, bei ninayowauzia hapa wana uwezo wa kuwauzia wananchi hadi Sh. 2,700 na wakapata faida, tunatakiwa kupata faida kidogo ili tusimkandamize mlaji," alisema Gullamal.

Mkazi wa Dodoma, Fideles Timothy, alisema wanashangazwa na kitendo cha kuuziwa sukari kilo moja kwa Sh. 3,000 hadi 5,000 na ameiomba serikali kuwachukulia hatua wafanyabiashara wa aina hiyo.

Hata hivyo, aliiomba serikali kuharakisha kufikishwa bidhaa hiyo waliyotangaza kwamba imeingia nchini ambayo anadai kuwa itapunguza makali bei ilivyo sasa.

Mfanyabiashara wa sukari kwa bei ya rejareja, Antonia Kessy, alisema kinachosababisha kuuza bidhaa hiyo zaidi ya Sh. 3,000 ni kuongezekana gharama za ufanyaji wa biashara.

Alisema sio wote wana usafiri wa kusafirishia bidhaa hizo bali wanakodi kwa ajili ya kuchukulia mzigo huo.





## Taratibu kuwapa ardhi wawekezaji zawekwa wazi

**Na Grace Mwakalinga, MBARALI**

VIONGOZI wa vijiji wameshauriwa kufuata taratibu za kisheria katika kugawa ardhi kwa wawekezaji ikiwamo kushirikisha wananchi badala ya kujiamulia wenyewe ili kuepuka kuibua migogoro kati ya wananchi na wawekezaji.

Ushauri huo ulitolewa juzi na Ofisa Mipango Miji kutoka katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Enock Kyando, alipokuwa akizungumza na Nipashe hatua mbalimbali walizozichukua katika kukabiliana na migogoro ya ardhi.

Kando ambaye ni Mjumbe wa Kamati Maalum ya uelimishaji wananchi kuhusu umuhimu wa uhifadhi na ujirani mwema, alisema Mkutano Mkuu wa Kijiji ndio wenye mamlaka ya kugawa ardhi ya kijiji.

Alisema kazi ya viongozi wa vijiji hasa ofisa mtendaji na mwenyekiti ni kupokea maombi ya wanaotaka kupewa ardhi na kuitisha mikutano ya vijiji ili wananchi wajadili na kuridhia ama kutoridhia kugawa ardhi yao kulingana na uhitaji.

"Msimamizi Mkuu wa ardhi ya kijiji ni wanakijiji wenyewe na ndio wanaotakiwa kuamua kumpa mtu mwingine ardhi yao kwa ajili ya matumizi ambayo wataona wao inafaa, kiongozi ukifanya maamuzi mwenyewe unasababisha migogoro," alisema Kyando.

Alisema kwa mujibu wa sheria ya ardhi, kijiji kinaruhusiwa kugawa ardhi isiyozidi hekta 50 kwa mtu mwingine na kwamba ikizidi ukubwa huo zipo mamlaka zingine ambazo zinahusika na hivyo mhitaji wa ardhi hiyo atatakiwa kuziona.

Kuhusu mpango wa matumizi bora ya ardhi, Kando alisema kila kijiji kinatakiwa kuwa na matumizi bora ya ardhi kwa maelezo kuwa utaratibu huo unasaidia kuondoa migogoro ya ardhi kwa kuepusha mwingiliano wa shughuli za kibinadamu.

Ofisa Ardhi wa Wilaya ya Mbarali, George Mwaijobelo, alisema wilaya hiyo imekuwa ikikabiliwa na migogoro mingi ya ardhi kutokana na vijiji vingi kutokuwa na matumizi bora ya ardhi.

Alisema kutokana na elimu ambayo kamati yao inaitoa kwa wananchi baadhi ya vijiji vimeanza kuwa na uelewa na kwamba vijiji hivyo vimeanza kupanga matumizi bora ya ardhi.

"Ardhi yetu haiongezeki, lakini binadamu tunaongezeka na mifugo yetu inaongezeka, kwa hiyo ni lazima tuwe na matumizi bora ya ardhi kulingana na shughuli zetu za kiuchumi na kijamii," alisema Mwaijobelo.

Alisema baadhi ya maeneo yanatakiwa kutengwa kwa ajili ya kilimo, makazi, kuchungia mifugo na shughuli zingine za kijamii ikiwamo maeneo ya viwanda na taasisi za serikali.

# Mwakyembe amwaga vifaa vya mil. 9/- vita ya corona

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

VIFAA vya kujikinga na maambukizo ya ugonjwa wa Covid-19 vyenye thamani ya shilingi milioni tisa vimekabidhiwa kwa uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya ili kuongeza nguvu katika mapambano dhidi ya ugonjwa huo.

Vifaa hivyo ambavyo ni ndoo 500 za kunawia mikono na sabuni za miche maboksi 100 na mabeseni 50, vilitolewa jana na Mbunge wa Jimbo la Kyela, Dk. Harrison Mwakyembe ambaye ni Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo.

Akikabidhi msaada huo kwa niaba ya Dk. Mwakyembe, Katibu wake Aman Mwakipesile alisema msaada huo utasaidia kukabiliana na ugonjwa huo hatari wa homa kali ya mapafu.

Mwakipesile alisema vifaa hivyo vitagawiwa kwenye maeneo mbalimbali ya kutolewa huduma kama vituo vya afya, masoko, stendi za mabasi katika kata zote na baaadhi ya mitaa ya maeneo ya mjini.

"Mbunge alifikia hatua ya kutoa misaada hiyo, baada ya kuona ugonjwa unashamiri kwenye maeneo mengi nchini, hivyo akaona atoe msaada kwa wananchi wake ili nao wajikinge," alisema Mwakipesile.

Akipokea msaada huo, Mkuu wa Wilaya ya Kyela, Claudia Kitta, alimshukuru Dk. Mwakyembe kwa kushirikiana na wadau wengine kwa madai kuwa wameongeza nguvu kubwa katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa corona.

Pia aliipongeza Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya kwa kuhakikisha eneo la Mpaka wa Tanzania na Malawi, Kasumulu linakuwa salama na kwamba hadi sasa hakuna mgonjwa yeyote wa Covid-19 aliyeripotiwa.

Akizungumza kwa niaba ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya, Katibu Mwenezi, Emmanuel Mwamlinge, alisema mbunge wao kafanya jambo jema kwa kujali maisha ya wapigakura wake.



Wachuuzi wa mboga wakiendelea na shughuli zao bila kuchukua tahadhari yoyote ya kukabiliana na maambukizo ya ugonjwa wa corona, ikiwamo uvaaji wa barakao wala kuweka ndoo za maji ya kunawa katika sehemu yao ya biashara, katika Mtaa wa Mtoni, Kata ya Ruanda, jijini Mbeya jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Wanakijiji wataka Tarura kuwaboreshea barabara

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

WAKAZI wa Kijiji cha Ipinda Kata ya Ihango katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wameomba serikali kupitia Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (Tarura), kuwaboreshea barabara katika kijiji hicho ili kuwarahisishia huduma za usafiri na usafirishaji wa mazao.

Wakizungumza na Nipashe, walisema barabara inayoanzia katika Gereza la Kawetere kwenda katika kijiji hicho ni mbovu na haipitiki mwaka mzima, hivyo wanaiomba Tarura itengeneze ili kurahisisha shughuli za usafiri kipindi hiki cha mavuno.

Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Mathias Mayemba, alisema barabara hiyo ambayo inawaunganisha na barabara kuu ya Mbeya- Chunya ni muhimu kwa ajili ya huduma za kijamii.

Mayemba alisema huduma nyingi wanategemea katika Jiji la Mbeya, lakini tatizo ni usafiri kwa maelezo kuwa kutokana na ubovu wa barabara hiyo hata gharama za usafiri ni kubwa.

"Kwa sasa mvua ikinyesha bajaji haiwezi kuingia hapa na ukitaka kutumia pikipiki gharama yake ni kubwa sana ukilinganisha na uchumi wetu... sasa tunaomba serikali itusaidie maana kipande hiki hakifiki hata kilomita mbili," alisema Mayemba.

Alisema serikali imewasaidia kuimarisha sekta ya elimu katika kijiji hicho kwa kuiboresha Shule shikizi ya Msingi Ipinda pamoja na kuwapelekea umeme na hivyo kilichobaki ni huduma ya barabara.


Ofisa Mtendaji wa Kijiji hicho, Fadhill Mwangupili, alisema kijiji hicho hakina zahanati kwa hiyo wajawazito huwa wanapata shida ya kwenda kujifungulia kwenye vijiji jirani.

Alisema kutokana na ubovu wa barabara hiyo wanahofu ya kuwapoteza wagonjwa wao endapo itatokea wakazidiwa usiku, hivyo akaomba wasaidiwe kuboreshewa barabara hiyo.

Mwangupili alisema uchumi wa wananchi wa kijiji hicho unategemea kilimo cha viazi mviringo, na kwamba kutokana na uchumi huo hawawezi kutengeneza barabara hiyo isipokuwa wanachangia shughuli zingine ndogo.

"Kwa sasa tunapambana kuboresha miundombinu ya shule yetu, tuliletewa fedha na Rais kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa na sisi tumejichanga kwa ajili ya ujenzi wa matundu ya vyoo," alisema Mwangupili.

Alisisitiza kuwa endapo wataboreshewa barabara hiyo kuna uwezekano hata soko la viazi wanavyozalisha likaboreka kwa maelezo kuwa kwa sasa bei zinakuwa ndogo kwa sababu wanunuzi wanasingizia ubovu wa barabara.



## SMZ yaanza ukarabati nyumba za kihistoria

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema imeanza kuzitambua na kuzifanyia ukarabati mkubwa nyumba za kihistoria za viongozi wakuu waasisi wa Zanzibar ikiwamo ya Rais wa Kwanza wa Zanzibar, hayati Abeid Amani Karume, iliopo Mwera.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Mohamed Aboud, alisema hayo wakati akitoa ufafanuzi kuhusu mikakati ya kutunza historia za viongozi wakuu walioleta ukombozi wa Zanzibar.

Alisema tayari kazi hiyo imeanza baada ya kutungwa sheria ya kuwalinda viongozi wakuu wa nchi na kupitishwa na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Aliitaja nyumba na sehemu aliyozaliwa hayati Abeid Amani Karume iliopo Mwera.

Hata hivyo, alisema kwa upande wa nyumba iliyopo Mwera, ukarabati wake umekwamba na Chama Cha Mapinduzi kimesema kazi hiyo itafanywa na wao ambao ndiyo dhamana.

"Nyumba ya Makumbusho iliyopo Mwera wenzetu wa Chama Cha Mapinduzi walisema wataifanyia wao kutokana na umuhimu wake na mchango wa kiongozi huyo katika harakati za ukombozi wa Mapinduzi ya Zanzibar," alisema.

Alisema nyumba ambayo imeanza kufanyiwa ukarabati ni iliyopo Mwembeladu ambayo ndiyo chimbuko la kuanzishwa kwa chama kilicholeta ukombozi Afro Shiraz Part (ASP).

Alisema serikali imeanza kutekeleza sheria ya kuwalinda na kuwatunza wastaafu walioleta ukombozi akiwamo Sheikh Thabit Kombo na marehemu Pili Khamis.

Pia, alisema kaburi la Rais mstaafu wa Zanzibar Sheikh Idriss Abdul Wakil, limefanyiwa ukarabati na kuwekewa uzio kwa kupata ushauri na ndugu wa familia.

"Sheria hiyo tayari imeanza kufanya kazi kwa kuyatunza makaburi ya waasisi wa mapinduzi na viongozi wastaafu akiwamo Makamu wa Rais na Waziri Kiongozi mstaafu marehemu, Dk .Omar Ali Juma," alisema.

# Sekta binafsi zaonywa kutumia corona kufukuza wafanyakazi

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

WATENDAJI wa Wizara ya Uwezeshaji Wanawake na Watoto pamoja na Wizara ya Biashara na Viwanda na Utalii, wametakiwa kukaa pamoja kulipatia ufumbuzi tatizo la wafanyakazi wa sekta binafsi ikiwamo wa hoteli kufukuzwa kazi kwa kisingizio cha ugonjwa wa corona.

Mwenyekiti wa Baraza la Wawakilishi, Mwanasha Khamis Juma, alisema hayo wakati akichangia bajeti ya wizara hiyo kuwa limejitokeza tatizo kubwa katika sekta binafsi wafanyakazi kufukuzwa na wengine kupewa likizo bila ya malipo kwa kisingizio cha kuwapo kwa ugonjwa wa corona.

Alisema utaratibu unaotumiwa na sekta binafsi ikiwamo hoteli za kitalii ni kinyume na sheria na wafanyakazi hao walitakiwa kujulishwa kuhusu tatizo liliopo na kupewa fedha za kujikimu.

Alieleza kuwa tayari wamepokea malalamiko mengi ya wafanyakazi kutoka sekta binafsi kuhusu kufukuzwa kazi katika kipindi hiki bila ya kupewa haki zinazostahiki kwa mujibu wa sheria.

"Wizara tatu zinazoshughulikia masuala ya wafanyakazi na utumishi zinatakiwa zikae pamoja na kulipatia ufumbuzi tatizo hili ili kuona wananchi wetu wanapata haki zao," alisema.

Naye Mwakilishi wa Jimbo la Shauri Moyo, Hamza Hassan Juma, alisema amesikitishwa kuona wafanyakazi wa kiwanda cha sukari kiliopo Mahonda, wamepewa likizo huku wakiambiwa ni tatizo la janga la ugonjwa wa corona.

Aliwataka waajiri katika sekta binafsi kuacha kutumia visingizio vya ugonjwa wa corona kwa ajili ya kuwapa likizo bila ya malipo na wengine kuwafukuza wakati wanapobaini mikataba yao kukaribia kumaliza muda ili wapoteze haki zao zote.

"Nimesikitishwa na uongozi wa kiwanda cha sukari Mahonda kuwapa likizo bila malipo wafanyakazi wake na kusitisha shughuli zote kwa kisingizio cha ugonjwa wa corona," alisema.

Kwa upande wake Mwakilishi wa Jimbo la Chakechake, Suleiman Sarhani, alisema wakati umefika sheria za kazi ifanyiwe marekebisho ili ziwalinde wafanyakazi wakati yanapotokezea majanga mbalimbali.

Alisema wafanyakazi wengi kutoka katika sekta binafsi ya hoteli wamepoteza ajira huku waajiri wakitumia kisingizio cha ugonjwa wa corona.

"Sheria za waajiri kutoka sekta binafsi zinahitaji marekebisho makubwa kwa sababu tumeona athari zake ni wananchi wetu wanaoathirika," alisema.

Naibu Waziri wa Uwezeshaji Wanawake, Wazee na Watoto, Shadya Suleiman, alikiri kuwapo tatizo la wafanyakazi katika sekta binafsi kupoteza ajira katika kipindi hichi cha ugonjwa wa corona.

Alisema suala hilo linafanyiwa kazi kuhakikisha wafanyakazi na waajiri wanakaa pamoja na kuona haki za wafanyakazi waliopoteza ajira au kwenda likizo bila ya malipo wanapata haki zao.



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi (kushoto), akijadiliana jambo na Mwakilishi wa Jimbo la Mwanakwerekwe, Abdallah Ali Kombo, nje ya ukumbi wa Baraza la Wawakilishi, mjini Zanzibar juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Waziri aahidi kupigia kampeni wanawake

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

WAZIRI asiye na wizara maalumu, Said Soud, amewataka wanawake kujitokeza kwa wingi kuwania nafasi za uongozi katika majimbo ya uchaguzi na kuahidi kuwapigia kampeni.

Soud alisema hayo wakati akichangia bajeti ya Wizara ya Uwezeshaji Wanawake na Watoto kwa mwaka wa fedha 2020-2021.

Alisema wanawake wameonyesha uwezo mkubwa wa kuongoza baada ya kukabidhiwa wizara mbalimbali nyeti pamoja na taasisi zake na kufanya vizuri.

Alisema, Rais wa Zanzibar Dk. Ali Mohamed Shein amewapa wanawake wizara nne muhimu zinazoshughulikia masuala ya elimu, biashara, mawasiliano na wanawake.

"Nampongeza kwa dhati Rais Shein kwa kuwaamini wanawake kushika nafasi nyeti, huku wakionyesha uwezo mkubwa wa kuziongoza na kupiga hatua kubwa ya maendeleo," alisema.

Alisema huu ni wakati muafaka wa wanawake kujitokeza katika majimbo ya uchaguzi kwa ajili ya kuchukua nafasi za uwakilishi katika vyombo vya kutunga sheria ikiwamo Bunge na Baraza la Wawakilishi.

"Huu ni mwaka wa uchaguzi mkuu kwa hivyo nawaomba wanawake wajitokeze kuwania nafasi za uongozi na kuingia katika vyombo vya kutunga sheria Bunge na Baraza la Wawakilishi na mimi naahidi kuwapigia kampeni wakihitaji," alisema.

Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi, Mgeni Hassan Juma, alisema wanawake wameonyesha mafanikio makubwa, katika baraza hilo, wapo wanawake watatu wanaongoza kamati za Baraza la Wawakilishi.

Alisema uwakilishi wa wanawake katika majimbo ya uchaguzi ni mdogo, huku kukiwa na Wawakilishi wanawake wanne pekee kutoka katika majimbo ya uchaguzi.

"Huu ni mwaka wanawake tunatakiwa kujitokeza kwa wingi kuwania nafasi za uchaguzi kupitia katika majimbo ya uchaguzi...wanaume sio kikwazo kwetu kwa kuwa tumeonyesha uwezo wa hali ya juu katika kuongoza."

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NAFASI ZA KAZI

**Anahitajika Boharia au (Store Keeper) na Muuguzi Msaidizi au (N/A)** Kwa anayehitaji apige simu namba: 0786 641 903/ 0716 172929


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676


## KAPALAMA AUCTION MART

### MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na dagaa Microfinance Ltd tutauza mali za wadaiwa Ndugu ALEXANDER JAMES CHAGGU na BUPE PETER NGUNULE tarehe 24/05/2020.

Gari namba T 561 DDS TOYOTA BREVIS na gari namba T 123 DEP TOYOTA PORTE.

**Mawasiliano:**
**0714 300 700.**

157484

## KUPOTEA KWA CHETI



**MWENDWA LIACHO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kuhitimu chuo cha ualimu chenye **No E.525/92** kilichotolewa na **CHUO CHA UALIMU MUSOMA** mwaka 1978.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Taarifa ya polisi: KNG/RB/481/2018

157473

## KUPOTEA KWA KADI

**THOMAS PIUS KAKANI**
**Anatangaza kupotea kwa kadi za pikipiki zenye namba za usajili zifuatazo**
**MC929CN-J,MC856CNK,MC743CNK,MC827CNK,MC757CNM,MC792CN-M,MC699CN-M,MC694CNM,MC707CNM,SU43642,SU43644,SU43643 –ARU/ARU/RB387023/202.**

**NA MC709CNM,MC711CNM –ARU/ARU/RB/378250/2020**

**Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.**

157485

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**LUKA DONASIAN MROSO** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 870 DHJ TOYOTA TOWNACE. Chassis namba CM550029537. Engine namba Z868GC.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **TAN/BUG/RB/382984/2020.**

157486

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**HAJI TWALIB REHANI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 634 DNR TOYOTA PASSO.** Chassis namba QNC10004211 8. Engine namba K31412416.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **DAR/BUG/RB/304017/2020.**

157482

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO (W)-BOMANI

WILAYA YA IRINGA

**KUITWA SHAURINI**

SHAURI LA MADAI. 16/2020
MDAI…..AIDAN GERVAS NYUMILE
DHIDI YA
MDAIWA…..HALUNA MDUGE

Shauri tajwa hapo juu limefunguliwa katika mahakama hii, na mdai dhidi yako mdaiwa.

Hivyo unaamriwa wewe mdaiwa mpopote pale ulipo kuhudhuria hapa mahakamani tarehe 21/7/2020 saa 2:30 asubuhi bila kukosa kwaajili ya kujibu madai hayo. Na kwakuwa siku hiyo ni siku ya kusikiliza shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako kwaajili ya kujitetea.

Usipofika bila taarifa shauri litasikilizwa upande mmoja na hukumu kutolewa.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 21/5/2020.

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO BOMANI
IRINGA.

157479

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA
USIMAMIZI WA MIRATHI
(S.M.M.1984 NYONGEZA)
YA 5 KANUNI YA 2

Katika mahakama ya mwanzo: MJINI-MOROGORO

Usimamizi wa mirathi No;127/2020

Ombi la **MARIA C. MTAITA** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **EMERENSIANA C. NGOWI**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe **25/06/2020** kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 21/05/2020.

Sahihi ya Hakimu
HAKIMU
MOROGORO

157480

---

**IN THE DISTRICT DELEGATE OFDODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATIONCAUSE**
**NO.33.2020**
**In the matter of the Estate of the LATE SECHELELA STANLEY MBOGONI of Kisasa within Dodoma city**
**And**
**In the matter of the Application for letters of Probate and Administration of estate by ROSEMARY MLAY**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules GN 369 of 1963)**

All persons claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of prob3ate (or letters of Administration) is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before 17/06/2020.

Dated at Dodoma this 11th day of 05/2020

Presented for filling this 08/05/2020

RESIDENT MAGISTRATE

157471

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**THE SILOAM MINISTRY INTERNATIONAL** inatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 609 AEA TOYOTA RAV 4 RANGI YA SILVER.** Chassis namba 8XA110278203.

Engine namba 3520022801.

**Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.**

**Taarifa ya Polisi: DSM/PHQ/RB/354395/2020.**

157478

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**DOTTO LAZARO NICHORAUS** amepotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 513 DFB** aina yake **JEEP-CHEROKEE** yenye engine namba **JNKPUD22UO7123** na chassis namba **JNKPUD22UO7.**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **MOR/MOR/RB/394452/2020.**

157481


Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Nipashe
MWANGA WA JAMII



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Trump kuitisha mkutano wa ana kwa ana wa G7

**WASHINGTON,** Marekani

RAIS wa Marekani, Donald Trump, amesema huenda akaitisha mkutano na wakuu wa kundi la mataifa saba yenye nguvu zaidi kiuchumi duniani (G7), katika makazi yake ya mapumziko ya Camp David, licha ya mzozo unaoendelea wa virusi vya corona.

Trump aliandika kwenye ukurasa wake wa twitter kuwa, kurejea kwenye hali nzuri na kusema huenda ataitisha mkutano huo mwezi Juni, badala ya kufanya kwa njia ya video kama ilivyopendekezwa awali.

Alisema mataifa wanachama pia yameanza kuimarika na hiyo ni ishara njema. Kansela wa Ujerumani, Angela Merkel, alisema atasubiri aone kile kitakachotokea huku Rais wa Ufaransa, Emmanuel Macron, akisema atahudhuria iwapo mazingira ya kiafya yataruhusu.

Wakati Rais Trump akisema uwezekano huo ni ishara ya mambo kurejea katika hali ya kawaida, Brazil imeripoti idadi ya juu kabisa ya vifo, wakati janga hilo likiliathiri vibaya kabisa taifa hilo la Amerika ya Kusini. **DW**

## Upigaji kura Burundi wakamilika salama

**BUNJUMBURA,** Burundi

UPIGAJI kura nchini Burundi umemalizika salama na kwa utulivu hapo, licha ya fukuto la machafuko ya kisiasa, janga la virusi vya corona huku upinzani nao ukizituhumu mamlaka kwa udanganyifu.

Rais Pierre Nkurunziza ambaye serikali yake mara kwa mara imeshutumiwa kwa ukiukaji wa haki, hatimaye ataondoka madarakani baada ya miaka 15.

Kiongozi wa upinzani, Agathon Rwasa hata hivyo alisema waangalizi wa uchaguzi huo uliofanyika juzi nchini humo kutoka chama chake walifukuzwa kwenye vituo vya kupigia kura.

Rwasa aliliambia Shirika la Habari la Reuters kwamba itakuwa vigumu kwao kukubaliana na matokeo kwa kuwa pamoja na udanganyifu mkubwa na waangalizi wao kufukuzwa vituoni, hawajaweza kushuhudia zoezi la kuhesabu kura. Serikali haikuzungumza chochote ilipoombwa kuzungumzia madai hayo. **DW**

# Watoto 115 wazaliwa na wanawake wenye corona

**MUMBAI,** India

WATOTO 115 wenye afya wamezaliwa kutoka kwa wanawake wenye maambukizo ya virusi vya corona katika mji wa Mumbai nchini India.

Watatu kati ya watoto hao, walizaliwa na wanawake wenye virusi katika hospitali kuu ya Manispaa ya Lokmanya Tilak, kipindi cha mwezi mmoja uliopita.

Awali, walipatikana na corona, na baadae vipimo vya madaktari viliyonyesha kuwa hawakuwa na virusi, walisema madaktari.

Wanawake wengine wawili wajawazito walifariki dunia hospitalini, akiwamo mmoja ambaye alikufa kabla ya mtoto wake kuzaliwa.

Huku kukiwa na watu takriban 24,000 walioripotiwa kuambukizwa corona na zaidi ya vifo 840 hadi sasa, mji huo mkuu wa Mumbai maarufu kwa biashara na burudani umekuwa ni kitovu cha corona.

**Timu ya madaktari 65 na wauguzi 24 wamekuwa wakiwatibu wanawake walioambukizwa corona katika vitanda maalum 40.**

Zaidi ya nusu ya watoto walizaliwa na wanawake walioathiriwa hospitalini, katika hospitali ya Sion walizaliwa kwa njia ya upasuaji na waliosalia wakizaliwa kwa njia ya kawaida, walisema maofisa.

56 kati yao walikuwa ni wa kiume na wa kike ni 59. Wanawake 22 kati yao waliletwa kutoka katika hospitali nyingine na haijawekwa wazi ikiwa wengi wao walipata maambukizi hayo nyumbani, sehemu nyingine au hospitalini.

Timu ya madaktari 65 na wauguzi 24 wamekuwa wakiwatibu wanawake walioambukizwa corona katika vitanda maalum 40.

Huku kukiwa na idadi kubwa ya maambukizo, hospitali inapanga kuongeza vitanda vingine 34 kwa ajili ya wanawake wajawazito wenye maambukizo ya corona.

Wanawake hao walijifungulia kwenye vitanda sita vya kujifungulia katika vyumba vitatu vya upasuaji na wauguzi na madaktari wa nusu kaputi wanatumia mavazi ya kujikinga dhidi ya maambukizi ya corona.

"Tunabahati kuwa wengi miongoni mwa wanawake waliopatwa na maambukizo kwa sasa hawaonyeshi dalili yoyote kabisa ya virusi vya corona," Mkuu wa Kitengo cha Wanawake katika hospitali hiyo, Dk. Arun Nayak alisema.

Alisema baadhi yao walikuwa na homa na waliripoti kukosa pumzi na kwamba waliwatibu na kuwaruhusu waende nyumbani baada ya kujifungua. **BBC**



Kimbunga kikali kimeikumba India na Bangladesh na kusababisha madhara makubwa jana. Taarifa zinaelezea kwamba watu wasiopungua 22 wamefariki dunia. **PICHA:AFP/NASA**

# Waathirika 106,000 corona waripotiwa saa 24

**GENEVA,** Uswizi

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO), imesema waathirika wapya 106,000 wa virusi vya corona wameripotiwa katika shirika hilo ndani ya kipindi cha saa 24 zilizopita.

Kutokana na hilo, limeonya janga hilo bado ni safari ndefu licha ya kwamba wanaoathirika wanaendelea kuongezeka kote duniani kila siku huku idadi ya jumla ikikaribia kufika milioni tano.

Mkurugenzi Mkuu shirika hilo, Tedros Ghebreyesus ameonesha wasiwasi wake kuhusu kuongezeka kwa maambukizo katika mataifa ya kipato cha chini na cha wastani.

Idadi hiyo ya kusikitisha ya karibia watu milioni tano inafikiwa chini ya wiki mbili baada ya kurekodiwa maambukizo milioni nne kote duniani.

Wataalamu wameonya kwamba idadi kamili ya maambukizo huenda ikawa ya juu zaidi na ya wanaopimwa ni ya chini katika nchi nyingi ambazo wanaficha taarifa zao.

Zaidi ya watu 326,000 wanakadiriwa kuwa wamekufa kwa corona kote duniani kulingana na Chuo Kikuu cha Johns Hopkins.

Marekani bado ndiyo iliyoathirika zaidi ikiwa na walioambukizwa milioni 1.5 na idadi ya waliokufa ikifikia 92,000.

"Katika kipindi cha saa 24 zilizopita, kumekuwa na maambukizo mapya 106,000 ambayo yameripotiwa kwa WHO ambayo ni makubwa zaidi kuandikishwa kwa siku moja toka janga la corona lianze," Dk. Tedros aliwaeleza wanahabari Jumatano jioni.

"Karibia theluthi mbili ya walioathirika wameripotiwa katika nchi nne pekee," aliongeza.

Dk. Tedros baadae alionya dunia kwamba safari ya kupambana na janga hili bado ni ndefu, onyo ambalo linatolewa wakati ambao mataifa kadhaa kama vile Marekani imeanza kulegeza masharti.

Mkurugenzi wa masuala ya dharura wa shirika hilo, Dk. Mike Ryan, alizungumza na wanahabari dhidi ya matumizi ya dawa za malaria ya chloroquine na hydroxychloroquine zinazohusishwa na ugonjwa wa corona.

Hilo linatokea baada ya Rais Marekani, Donald Trump kusema amekuwa akinywa dawa ya inayokusudiwa kutibu malaria kama njia moja ya kujikinga dhidi ya corona, licha ya onyo kutoka kwa maofisa wake wa afya kuhusu matumizi ya dawa hiyo.

"Hadi kufikia sasa, dawa ya kutibu malaria ya hydroxychloroquine au chloroquine bado haijathibitishwa kuwa salama katika kutibu ugonjwa wa corona kama njia ya kukabiliana na ugonjwa huu," Dk. Ryan alisema. **BBC**

# MAGUIRE: NAJISIKIA SALAMA KURUDI MAZOEZINI



**MANCHESTER,** England

NAHODHA wa Manchester United, Harry Maguire amesema alijihisi "salama sana" wakati miamba hao wa Ligi Kuu England waliporudi kuanza mazoezi baada ya mlipuko wa virusi vya corona.

United walirudi kwenye mazoezi pale kwenye kambi yao ya Carrington Jumatano baada ya timu za Ligi Kuu England kuwashiwa taa ya kijani kuanza mazoezi ya makundi Jumanne.

Msimu wa Ligi wa 2019-20 ulisimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona Machi mwaka huu wakati United walikuwa nafasi ya tano na kupitwa pointi tatu nje ya nafasi ya kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya, baada ya kucheza mechi 29.

Maguire alifurahishwa na kurudi tena mazoezini na klabu yake, akiiambia tovuti ya timu hiyo: "Nilikuwa kama mgeni kwa miezi michache, lakini sasa mambo yako vizuri na inaonekana mazingira ni salama sana.

"Ni siku yetu ya kwanza mazoezini, lakini hali inaonekana kuwa salama na kila mmoja anatarajia mambo yatakuwa mazuri zaidi."

# Iniesta: Barcelona ya Messi ilitakiwa kubeba Uefa nyingi

**BARCELONA,** Hispania

ANDRES Iniesta anaamini Lionel Messi ni bora duniani na anahisi Barcelona ilitakiwa kushinda mengi zaidi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya ikiwa na nahodha huyo.

Messi amejiimarisha yeye mwenyewe kama mmoja wa wachezaji bora wa wakati wote wa soka akiwa ndiye mchezaji anayeongoza kwa ufungaji mabao katika historia ya Barca na mshindi mara sita wa Ballons d'Or.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 mara kwa mara amekuwa akipambanishwa na nyota wa Juventus na mkali wa zamani wa Real Madrid, Cristiano Ronaldo.

Lakini gwiji wa Barca, Iniesta – ambaye kwa sasa anacheza katika klabu ya Vissel Kobe ya nchini Japan – anamuona mchezaji mwenzake huyo wa zamani ndio namba moja kwa ubora duniani.

"Anafanya mambo kuwa tofauti kwa kila njia," amesemwa mkongwe huyo wa timu ya taifa ya Hispania, Iniesta mwenye umri wa miaka 36, akiiambia Ole.

"Anauwezo wa kufunga hat-trick huku pia akitoa pasi za mwisho nyingi, kama ukitaka kufurahia kumtazama, mwangalie ukiwa jukwaani."

Tangu aanze kutamba pale Barca mwaka 2004, Messi ameisaidia kutwaa mataji manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na mataji 10 ya LaLiga.

Iniesta amesema Barca ilitakiwa kushinda mataji mengi zaidi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa uwepo wa Messi.





# *Martinez amtaja Hazard tuzo ya Ballon d'Or*

**MADRID,** Hispania

EDEN Hazard anaweza kushinda Ballon d'Or akiwa Real Madrid, kwa mujibu wa Kocha Mkuu wa Ubelgiji, Roberto Martinez.

Hazard aliondoka Chelsea na kujiunga Madrid kwa ada ya euro milioni 100 mwanzoni mwa msimu wa 2019-20, lakini nyota huyo wa Ubelgiji amekuwa na wakati mgumu kule kwenye Uwanja wa Santiago Bernabeu.

Majeruhi ya mara kwa mara, yamemfanya Hazard kucheza mechi 15 tu kwa klabu hiyo ya mji mkuu wa Hispania, ambapo hajacheza tangu Februari 22, mwaka huu kutokana na kuvunjika kifundo cha mguu.

Lakini kocha wake, Martinez - ambaye ameongeza mkataba wa kuinoa Ubelgiji Jumatatu, anatarajia vitu vikubwa kutoka kwa Hazard.

"Anaweza kushinda Ballon d'Or akiwa na Real Madrid, bila shaka yoyote," amesema Martinez akiiambia Cadena Ser.

"Wakati mwingine inakuwa vigumu kuanza katika klabu mpya, kwanza unatakiwa kwanza kuelewa mazingira yalivyo na hivyo ndio ilivyomtokea pale Real Madrid.

"Nina uhakika Eden atafanya makubwa katika klabu ya Real Madrid na kuna nafasi ya yeye kufikia kwenye kiwango cha daraja la juu kabisa kwenye mafanikio binafsi."

# Emerson afunguka kurudi Serie A

**LONDON,** England

EMERSON Palmieri amesema anaweza kurudi kule Serie A, ingawa beki huyo wa pembeni wa Chelsea amesisitiza hana haraka ya kuondoka Stamford Bridge.

Nyota huyo wa Chelsea, Emerson amekuwa akihusishwa na kutakiwa na mabingwa wa Serie A, Juventus na Inter Milan baada ya kuondoka AS Roma na kwenda Ligi Kuu England mwaka 2018.

Emerson alitumia miaka miwili na nusu akiichezea Roma na sasa mchezaji huyo aliyeichezea Timu ya Taifa ya Italia mara saba anaweza kufungua milango ya kurudi Serie A.

"Nilikuwa na furaha wakati nikicheza Serie A, ikiwamo tamaduni, ndio maana nilichagua kuichezea Timu ya Taifa ya Italia," amesema akiiambia Sky Sport Italia.

"Kurudi Serie A kunaweza kutokea, lakini bado nina mkataba na Chelsea na sina haraka ya kwenda kokote.

"Nimekuwa na wakati wa kuvutia pale Chelsea, kwa mara ya kwanza kulikuwa na (Antonio) Conte, hivyo ilikuwa rahisi kuelewana na kocha huyo Muitaliano."





# JUVENTUS HAIJATOA OFA KWA JORGINHO

**LONDON,** England

WAKALA wa Jorginho, Joao Santos, amesisitiza Juventus haijamuulizia nyota huyo wa Chelsea, ingawa alikubali kuwa mchezaji yeyote angependa kuwachezea mabingwa hao wa Serie A.

Juve iliripotiwa kwamba inataka kumuunganisha kocha wao, Maurizio Sarri na kiungo Jorginho pale Turin - ambapo wawili hao walifanya kazi pamoja katika klabu za Chelsea na Napoli.

Jorginho ametajwa kama anaweza kuwa mrithi sahihi wa Miralem Pjanic, ambaye amekuwa akihusishwa kutakiwa na mabingwa wa LaLiga, Barcelona na vinara wa Ligue 1, Paris Saint-Germain.

Alipoulizwa kuhusu majaliwa ya Jorginho na kuripotiwa kuwaniwa na Juve, Santos aliiambia redio Kiss Kiss: "Juventus ni moja ya timu kubwa Ulaya na mchezaji yoyote angependa kuichezea.

"Sijasikia kutoka kwa (Mkurugenzi wa Michezo) Paratici, hajanipigia mimi. Jorginho amebakisha miaka mitatu kwenye mkataba wake na Chelsea, anafanya vizuri kule London.

"Nimesoma kuhusu kuhusishwa na Juve kupitia kwenye magazeti tu, lakini hakuna mawasiliano yoyote."

Santos aliongeza: "Narudi, Juventus ni moja ya klabu kubwa ya soka duniani."

# *Suarez amwambia Lautaro abakie Inter Milan*

**BARCELONA,** Hispania

NYOTA wa zamani wa Inter Milan na mshambuliaji wa Barcelona, Luis Suarez, anaamini Lautaro Martinez anatakiwa kubakia kwa miamba hao wa Serie A.

Martinez mwenye umri wa miaka 22, ameripotiwa kuwaniwa kwa udi na uvumba na Barca baada ya kufunga mabao 16 katika mechi 31 kwa Inter msimu huu.

Mshindi huyo wa Ballon d'Or mwaka 1960, Suarez alikwenda upande mwingine wakati wake akiwa kijana, akitoka Barca na kutua Inter mwaka 1961.

Mchezaji huyo wa zamani wa timu ya taifa ya Hispania amesema kama angekuwa yeye ni Martinez, angebakia pale San Siro.

"Kama ningekuwa mimi, singebadili timu," alisema akiliambia gazeti la La Gazzetta dello Sport Jumatano.

"Kufanya maamuzi ya ama kubakia au kuondoka, ni vigumu, ingawa kama (Lionel) Messi amemwita itakuwa rahisi kufikiria kuhusu hilo.

"Hata hivyo, tunamzungumzia kijana ambaye bado ni mdogo sana, na bado ana muda wa kutosha wa kukabiliana na changamoto nyingi katika siku za usoni."

Martinez anaweza kuungana na Messi pale Barcelona, ambapo wamekuwa wakicheza kwa pamoja kwenye timu ya taifa ya Argentina.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# CEBALLOS ATAKA KUREJEA MADRID

**Mhispania huyo afunguka ameiva na yuko tayari kwenda kuwania namba Madrid...**

**LONDON,** England

KIUNGO wa Timu ya Taifa ya Hispania, Dani Ceballos (23), amesema baada ya kumaliza mkataba wake wa mkopo kwenye kikosi cha Arsenal mwishoni mwa msimu huu, anarejea Real Madrid.

**Kiungo huyo alijiunga na Arsenal kwa mkopo na aling'ara katika baadhi ya mechi chache alizoichezea klabu hiyo ya London Kaskazini kabla ya kuweka pembeni Novemba mwaka jana kwa sababu ya maumivu aliyopata ya nyama za paja.**

Majeraha hayo yalimfanya Mhispania huyo akae nje kwa miezi mitatu na kumsababisha ashindwe kutimiza malengo yake ya kukaa hapo Emirates.

Hata hivyo Ceballos alirejea kufanya kazi vema chini ya Mikel Arteta ambaye alifikiria kumweka kwenye kikosi cha kwanza kwenye mechi tatu zilizochezwa kabla ya kuingia kwa janga la corona.

Gazeti la The Mirror limeandika Arsenal inataka kuona Ceballos anabakia jijini London Kaskazini, lakini Mhispania huyo ameshaweka wazi anataka kuondoka.

"Mimi ni mchezaji halali wa Real Madrid, na kila mchezaji duniani anataka kuichezea Real Madrid," alisema Ceballos wakati akizungumza na Kituo cha TVE cha Hispania Jumatano wiki hii.

"Nina mkataba wa miaka mitatu na klabu hiyo na ndiyo timu inayojipanga kupata mafanikio."

Mkataba wa kiungo huyo mwenye umri wa miaka 23 na The Gunners unatarajiwa kumalizika Juni 30, mwaka huu, lakini Arsenal inaonekana inataka kuiomba Real imbakishe mchezaji huyo hadi mwisho wa msimu huu.

Lakini inaonekana mara msimu huu utakapomalizika, Ceballos atasisitiza kwenda kupambana kusaka namba katika kikosi cha Real.

Inaelezwa hakuna makubaliano yoyote ya kumuuza kiungo huyo yaliyofikiwa kwenye mkataba wa Ceballos wakati anajiunga na Arsenal majira ya joto mwaka jana.

"Nina furaha bado nina mkataba na Real Madrid," Ceballos aliongeza.

"Nina umri wa miaka 23. Sasa ninajiona ni mchezaji kamili na nimejiandaa kukabiliana na changamoto yoyote itakayokuwa mbele yangu nitakapokuwa."

## ZISIKUPITE

### SANE KUPEWA JEZI NA. 10

MSHAMBULIAJI wa Manchester City na Timu ya Taifa ya Ujerumani, Leroy Sane (24), amewekewa jezi namba 10 ili atakapotua Bayern Munich ifikapo msimu ujao, aweze kuivaa. ***(Mirror)***

### MOSES HAKIJAELEWEKA

CHELSEA inapambana kushusha thamani ya Victor Moses kwa kushusha dau lake lakini Inter Milan bado inagoma kulipa pauni milioni 10.75 ambayo ndiyo thamani ya winga huyo wa Timu ya Taifa ya Nigeria mwenye umri wa miaka 29. ***(Sun)***

### JORGINHO AIKUBALI CHELSEA

WAKALA wa Jorginho (28), amesema kiungo huyo wa Timu ya Taifa ya Italia ana furaha kuendelea kubakia Chelsea na kuongeza bado hakuna mawasiliano yoyote yaliyofanyika na Juventus kuhusiana kumhitaji nyota huyo. ***(Metro)***

### BARCELONA, PSG VITANI

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer anataka kumbakisha klabuni hapo beki wa Timu ya Taifa ya Ureno, Diogo Dalot (21), licha ya mlinzi huyo kuwindwa na Barcelona na Paris St-Germain. ***(ESPN)***

### LIVERPOOL KUUZA WATATU

LIVERPOOL iko tayari kuuza wachezaji wake watatu katika majira ya joto ili kusaka pauni milioni 52 za kusaidia mchakato wa kumsajili mshambuliaji wa RB Leipzig na Timu ya Taifa ya Ujerumani, Timo Werner (24). ***(Athletic - subscription required)***

### CAKIR ATINGA SOKONI

GOLIKIPA wa Trabzonspor ya Uturuki ambaye anawindwa na Leicester City, Ugurcan Cakir (24) anatakiwa na Sevilla ya Hispania kwa dau la pauni milioni 18. ***(Leicester Mercury)***

### RASHFORD AMPOTEZA IGHALO

WAKATI Manchester United inaonekana kutaka kumbakisha straika, Odion Ighalo (30), ambaye yuko klabuni hapo kwa mkopo akitokea Shanghai Shenhua, lakini wanaoneka kutoendelea na mchakato wa kumpa mkataba wa kudumu Mnigeria huyo baada ya Marcus Rashford kuwa fiti. ***(Sky Sports)***

### LACAZETTE AKARIBIA ATLETICO

ARSENAL inajipanga kuridhia kubadilishana wachezaji kwa kuona Atletico Madrid inamsajili straika wake Mfaransa, Alexandre Lacazette (28) anatua Hispania na wao wanapata saini ya Thomas Lemar (24). ***(AS - in Spanish)***

### SANE KUKAMULIWA

VIGOGO wa Bundesliga, Bayern Munich wamemweleza mshambuliaji wa Manchester City, Leroy Sane kupunguza kiasi cha asilimia 30 katika dau lake ili kufanikisha usajili wa kutua Ujerumani katika dirisha la majira ya joto. ***(Bild, via Star)***

### PSG YACHEMKA KWA KALIDOU

PSG imejiondoa kwenye mbio za kuwania saini ya beki wa kati wa Napoli, Kalidou Koulibaly (28), kwa sababu ya thamani yake iliyotangazwa kuwa pauni milioni 63 na kuiacha Manchester United kuendelea na mchakato wa kumsajili nyota huyo raia wa Senegal ifikapo majira ya joto. ***(Le Parisien - in French)***

HABARI MICHEZO

## Namungo FC yafunguka Yanga inawavuruga

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Namungo FC, Thiery Hitimana, amesema tetesi za Yanga kutaka wachezaji wake 'kunamvuruga' katika kupanga mikakati ya usajili kuelekea msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Yanga inatajwa kufanya mazungumzo na wakala wa mshambuliaji wa Namungo, Bigirimana Blaise.

Hitimana ameliambia gazeti hili jana analazimika kutoa mapendekezo ya usajili kwa sasa ili kuwabakisha wachezaji wake kwa shinikizo linalotokana na tetesi za nyota wake kuwindwa.

Alimtaja Bigirimana ni mmoja wa washambuliaji tegemeo katika kikosi chake na yupo kwenye mipango ya usajili wa msimu mpya.

"Huu ni muda wa kufanya mapendekezo ila kwangu imekuwa ngumu, kwanza kuna taarifa za baadhi ya timu kutaka wachezaji wangu, hili bado linanipa hofu, nasubiri ligi itakapomalizika ndio nitaangalia," alisema Hitimana.

Aliongeza awali hakupanga kufanya mabadiliko makubwa katika kikosi chake lakini anajiandaa kukisuka upya endapo viongozi wa timu hiyo watashindwa kuwabakisha nyota hao wanaotakiwa na vigogo vya soka nchini.

## Wachezaji, viongozi kupimwa corona

**Na Faustine Feliciane**

BODI ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB), imesema itawafanyia vipimo vya corona wachezaji na viongozi wote kabla ya kuendelea kwa msimu huu wa ligi.

Mwenyekiti wa TPLB, Steven Mguto, alisema baada ya serikali kutangaza kurejea kwa Ligi Kuu, bodi hiyo imeanza kufanya tathmini kwa kukutana na Kamati ya Afya kuandaa maoni yatakayosaidia kurejea vema kwa michezo hiyo.

Mguto alisema suala la afya kwa wachezaji, viongozi na mashabiki katika kipindi hiki cha mlipuko wa virusi vya corona litazingatiwa na kupewa kipaumbele kikubwa.

"Bado mapendekezo mengine yanapokelewa kwa kamati maalum kabla ya urejeo wa ligi, bodi tunaendelea kuangalia namna bora ya kucheza michezo ya ligi, kikubwa tunataka kuona ligi zote zinamalizika," alisema Mguto.

Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, alisema michezo itarejeshwa kwa mafungu na wamepanga kuanza na soka kwa ajili ya kumalizika Ligi Kuu, Ligi Daraja la Kwanza na mashindano ya Kombe la FA.

# SIMBA YAMWAGA VIFAA VYA CORONA MUHIMBILI

**Na Mwandishi Wetu**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Bara, Simba kwa kushirikiana na Taasisi ya Mo Dewji ya hapa nchini wamegawa vifaa na dawa mbalimbali katika Hospitali ya Rufani ya Taifa ya Muhimbili kwa ajili ya kupambana na maambukizo ya virusi vya corona (COVID 19).

**Sehemu nyingine ambazo misaada hiyo imepelekwa ni Taasisi ya Mifupa ya Moi na Taasisi ya Magonjwa ya Moyo ya Jakaya Kikwete.**

Mbali na dawa hizo, pia Simba na taasisi hiyo wametengeneza mabomba kwa lengo la kusaidia wagonjwa na ndugu wanaofika kwenye hospitali hiyo kusafisha mikono na maji tiririka.



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Senzo Mbatha (pichani), alisema jana kuwa klabu yao inafuraha kuona imeshiriki kupambana na ugonjwa huo kwa kusaidia jamii inayowazunguka.

Senzo alisema kwa uamuzi huo, Simba inaona faraja kushiriki katika mapambano ya ugonjwa huo ambao umetikisa dunia na kuongeza maisha yamebadilika kupitia janga hilo.

"Kwa niaba ya Simba na Bodi, ninafuraha kukabidhi vifaa hivi, ni msaada unaogusa watu, ni vizuri kuungana kushirikiana na watu, huu ni msaada wenye thamani kubwa na si suala la kuosha tu mikono," alisema Mbatha.

Alisema uamuzi wa kushiriki kutoa misaada haukuchukua mjadala na Simba inaahidi kuendelea kusaidia jamii na anaamini klabu nyingine pia zitaunga mkono zoezi hilo.

Mkuu wa Taasisi ya Mo Dewji, Barbara Gonzalez, alisema taasisi hiyo ilianza ujenzi wa mabomba ya kunawia tangu Machi, mwaka huu na wakaona si vibaya kushirikiana na Simba katika kufikia malengo yao.

Alisema bado taasisi hiyo na Simba itatoa vifaa vingine kwa ajili ya kuendelea kupambana na ugonjwa huo.



Mhudumu wa uwanja akipulizia mpira dawa ya kujikinga na virusi vya corona (Covid-19), kabla ya wachezaji wa Spurs hawajaanza mazoezi ya kujiandaa na mechi za Ligi Kuu England. **PICHA : MTANDAO**

## *Eymael kurejea kibaruani Yanga*

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Luc Eymael, anatarajiwa kurejea nchini wakati wowote kuanzia leo ili kuungana na kikosi chake baada ya kukamilika kwa maandalizi ya usafiri wa ndege.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya mtandao Luck alisema ameshafanya mawasiliano na uongozi ili kujua utaratibu mzima wa tiketi pamoja na ndege itakayomfaa kwa safari.

"Nimeshukuru kusikia ndege zimeanza kuruhusiwa kuja Tanzania, binafsi nimefarijika mipango ya safari ikikamilika nitarudi kuendelea na ligi," alisema Eymael.

Aliongeza kwa muda wote alipokuwa Afrika Kusini alikuwa akiwasiliana mara kwa mara na wachezaji wake kufahamu utekelezaji wa programu za mazoezi na hana wasiwasi na uwezo wao wa kurejea kumalizia msimu.

"Lengo ni kuipa mafanikio klabu yetu kwa kushika nafasi ya juu katika msimamo wa Ligi Kuu, tuombe taratibu zikamilike kila kitu kitakuwa sawa, " Eymael aliongeza.

Naye nahodha msaidizi wa Yanga, Juma Abdul, alisema anatamani kurudi uwanjani mapema ili kuendelea na majukumu yake.

Beki huyo alisema amekuwa na 'kiu' na mashabiki wake baada ya kukaa kwa muda mrefu bila kucheza, kutokana na ligi hiyo kusimamishwa ili kupisha maambukizo ya corona (COVID 19).

# Michezo

Ijumaa Mei 22, 2020

Nipashe




Ceballos ataka kurejea Madrid UKURASA 22




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Senzo Mbatha (kulia), akikabidhi msaada wa dawa za kujikinga na Covid -19 kwa ajili ya Hospitali ya Taifa ya Rufani ya Muhimbili, Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete na Taasisi ya Mifupa (MOI). Wengine kuanzia kushoto ni Mkuu wa Kitengo cha Huduma kwa Wateja Muhimbili, Dk. Tulizo Shemu na Mkurugenzi wa Tiba Muhimbili, Dk. Hedwiga Swai. **PICHA: SIMBA SC**

# LIGI KUU BARA YAREJEA RASMI

## Rais Magufuli atangaza michezo yote kufanyika kuanzia Juni Mosi, lakini mashabiki...

**Na Romana Mallya**

KIPENGA kimelia! Rais John Pombe Magufuli, ametangaza rasmi kufungua michezo yote nchini kuanzia Juni Mosi, mwaka huu lakini amesisitiza taratibu za mashabiki kushangilia zitatolewa kitaalamu na wizara husika.

**Rais Magufuli alitoa maagizo hayo jana katika Ikulu ya Chamwino jijini Dodoma wakati akiwaapisha viongozi mbalimbali aliowateua hivi karibuni.**

Magufuli alisema wizara zitakazotoa mwongozo wa namna ya kuruhusu mashabiki ni Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

"Kuna michezo ya jeshi, ni lazima watu wafanye michezo, taratibu za kushangilia na kuangalia zinaweza kupangwa vizuri na Wizara ya Afya pamoja na wizara husika ya michezo ili ule umbali kati ya mtu na mtu ukaendelee kuwapo katika kipindi hiki cha maambukizo," Magufuli alisema.

Alisema kutokana na maambukizo ya virusi vya corona kupungua hapa nchini, ameamua kufungua michezo kwa sababu anafahamu kila mtu anaipenda.

"Ninafahamu kila mmoja anapenda michezo hata wabunge wanakwenda kwenye michezo, nikwenye michezo, nilioouna, sina hakika kama kuna mwanamichezo aliyefariki hapa Tanzania kwa corona, kuwa na michezo kunasaidia kupambana na corona.

"Kuwa na michezo kunasaidia kupambana na corona na michezo ipo mingi, kila mmoja na mchezo wake, lakini michezo ni kitu kinachosaidia.

Kiongozi huyo aliongeza michezo ipo ya aina mbalimbali ikiwamo sanaa ya kuigiza, na uamuzi wa kujibana kwa kiwango cha juu si salama.

"Si lazima tusijibane sana, kukutana kutana huku kunajenga kinga za mwili hii, na hii itatusaidia kupambana na magonjwa, na si corona tu, hata na magonjwa mengine itatusaidia," aliongeza Magufuli.

Alisema pia ukifungia watu katika nyumba kwa siku nyingi, siku utakayowafunguliwa, kinga zao za mwili zitakuwa zimeshuka kwa asilimia 30.

"Nataka kuwahakikishia Tanzania tunaenda vizuri, tuko vizuri, na Mungu wetu ameendelea kutusimamia, tulianza na Mungu, nina hakika tutamaliza na Mungu, hakuna mahali popote taifa lililomtegemea Mungu likaenda kushindwa,... Mungu amejibu, amejibu maombi yetu, amejibu kwa kiasi kikubwa na amejibu kwa kishindo," alisema Magufuli.

Machi 17, mwaka huu Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alitangaza kusitisha mikusanyiko yote ikiwamo shughuli za michezo na matamasha ya muziki.

## Simba yaipiga 'dongo' Yanga

**Na Faustine Feliciane**

SIKU chache baada ya Yanga kutangaza kuanza mchakato wa mabadiliko ya uendeshaji wa klabu yao, watani zao, Simba wamewapongeza kwa hatua hiyo lakini wamewatupia 'dongo' kuacha kulalamika ovyo kuhusiana na matokeo ya uwanjani.

Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara, alisema kuwa ni jambo zuri kwa Yanga kufuata nyayo zao mfumo wa uendeshaji kuzitaka klabu nyingine kufanya mabadiliko hayo ili wasiachane mbali.

"Nawapongeza Yanga kuja huku tulipo sisi, lakini ni lazima mabadiliko yao yaende na mabadiliko ya fikra zao, waache mambo ya kulalamika ovyo wanapofanya vibaya, timu inayojiita klabu kubwa haipaswi kulalamika hovyo kwa matokeo ya uwanjani, lalamika kwa hoja na sio kila kitu kulalamika," alisema Manara.

Alisema mabadiliko hayo yatasaidia mchezo wa soka hapa nchini kuwa na ushindani na wanaamini yataongeza upinzani wao kwenye ligi na mashindano yote wanayoshiriki.

Yanga imezindua mchakato wa mfumo wa mabadiliko ya uendeshwaji ikiwa ni moja ya sera kuu iliyowaweka madarakani Mwenyekiti, Dk. Mshindo Msolwa na makamu wake, Frederick Mwakalebela.

## Mwamnyeto njia nyeupe Simba SC

**Na Saada Akida**

KOCHA Msaidizi wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, Selemani Matola amesema beki wa Coastal Union, Bakari Mwamnyeto ana nafasi katika kikosi cha kwanza cha Wekundu wa Msimbazi endapo atasajiliwa katika klabu hiyo.

Mwamnyeto ambaye bado ana mkataba wa mwaka mmoja na Coastal Union ya jijini Tanga, anatajwa kuwindwa na Simba na Yanga.

Akizungumza na gazeti hili jana, Matola alisema Mwamnyeto ni mmoja wa mabeki wachache wenye uwezo wa hapa nchini na endapo atatua Simba, ana hakika atapata nafasi ya kucheza mechi nyingi.

"Kama kweli atasajiliwa Simba, lazima atapata nafasi ya kucheza kutokana na uwezo wake anacheza mipira ya juu, pia ni mzuri katika mipira ya chini," alisema Matola.

Alisema mbali na uwezo wake pia beki huyo ni aina ya wachezaji 'mbegu' ya zamani ambayo kwa kizazi cha sasa kimepotea.

"Kutokana na uwezo wake huo, kwangu nina imani nyota huyo kupata nafasi ya kucheza ila tu atakapojitambua na kujituma baada ya kusajiliwa katika timu kubwa," Matola alisema.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042